MIFANO MAHSUSI

Inayofafanua Sheria dhidi ya Ufisadi nchini Kenya

TUME YA KUPAMBANA NA UFISADI YA KENYA

Kwenye Mstari wa Mbele dhidi ya Ufisadi

MIFANO MAHSUSI

SHERIA DHIDI YA UFISADI

Mifano Mahsusi

© Chapisho la Tume ya Kupambana na Ufisadi ya Kenya
Kitengo cha Huduma za Kuzuia Ufisadi
Idara ya Elimu

Tahadhari

Maoni na vielelezo katika Mifano hii Mahsusi ya Sheria dhidi ya Ufisadi nchini Kenya havidai kuwa fasiri timilifu au ya kimahakama kuhusu Sheria zinazofafanuliwa. Juhudi zote zimechukuliwa ili kurahisisha sheria hizi kwa wasomaji wote kwa jumla. Hata hivyo, chapisho hili, kivyake sio mbadala wa sheria za kupambana na ufisadi nchini Kenya. Watumiaji wa chapisho hili, hivyo basi wanahimizwa kuzisoma sheria zenyewe vilevile. Wahusika na mifano yote inayopatikana katika chapisho hili ni ya kubuni na inatumika kwa sababu za kufafanua tu.

©Tume Ya Kupambana na Ufisadi ya Kenya
Kitengo cha Huduma za Kuzuia Ufisadi
Idara ya Elimu

YALIYOMO

DIBAJI....ii
MFANO A....1
Maswali:....2
MFANO B....4
Maswali:....5
MFANO C....7
Maswali:....8
MFANO D....10
Maswali:....11
MFANO E....14
Maswali:....15
MFANO F....17
Maswali:....17
MFANO G....19
Maswali:....19
MFANO H....21
Maswali:....22
MFANO I....24
Maswali:....25
MFANO J....29
Maswali:....30
MFANO K....32
Maswali:....33
MFANO L....34
Maswali:....35
MFANO M....37
Maswali:....37
MFANO N....40
Maswali:....41
MFANO O....44
Maswali:....44
MFANO P....47
Maswali:....47
MFANO Q....51
Maswali:....52
MFANO R....55
Maswali:....55
MFANO S....57
Maswali:....57
MFANO T....58
Maswali:....58
MFANO U....60
Maswali:....60
ADHABU....60

DIBAJI

Tume ya Kupambana na Ufisadi ya Kenya imejitolea mhanga kuhakikisha kuwa wakenya wengi iwezekanavyo wanaelewa kwa ukamilifu kuhusu ufisadi, athari zake kwa jamii na manufaa ya kujiepusha na uovu huu. Kwa hivyo, Tume imechapisha kitabu hiki ambamo mifano mbalimbali imetafitiwa ili kuonyesha jinsi ufisadi na utovu wa maadili vinavyojitokeza waziwazi katika maisha yetu halisi. Utafiti wa matukio haya utakuwa kama mwongozo kwa watumishi wa umma, wananchi binafsi na umma kwa jumla kutambua, kufahamu, kukabili na kujua jinsi ya kutatua jambo lolote linalohusu ufisadi na maadili yanayotatiza katika kazi na kuingiliana kwao.

Mifano iliyotafitiwa katika toleo hili imepangwa kwa njia ambayo inamhitaji msomaji kutambua na kutafakari juu ya maswala muhimu yanayojitokeza. Kwa njia hii, msomaji anaweza kufahamu ufisadi na utovu wa maadili kama inavyoelezewa katika sheria na pia katika maisha halisi tunayoishi kama Wakenya. Kisha, msomaji anachochewa kutafuta njia mwafaka za kutatua matatizo yaliyo katika kila tukio mahsusi. Tunapoendelea kujitahidi kuchapisha vitabu zaidi vinavyoeleweka kwa urahisi kuhusu jinsi ya kupambana na ufisadi, kwa kutumia mbinu zinazoeleweka kwa urahisi na vielelezo, Tume inatarajia kuwa Wakenya zaidi watajifunza na kuhusika vilivyo kwa ujasiri katika vita dhidi ufisadi. Kama tunavyoendelea kusisitiza, vita dhidi ya ufisadi vitafua dafu wakati Wakenya wote watakapojitwika jukumu la kibinafsi la kupambana na ufisadi.

Ili kufaidika vilivyo kutokana na matukio yanayoelezwa katika kitabu hiki, ni muhimu msomaji aelewe asili, aina na jinsi watu hushiriki ufisadi na kukiuka maadili kama inavyoelezwa katika sheria za Kenya na vitengo vingine vya kisheria. Kwa hivyo, Tume hii imerahisisha sheria za kupigana dhidi ya ufisadi na kuchapisha vitabu ambavyo vimetolewa bila malipo kwa wasomaji. Vitabu hivi ni pamoja na Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi 2003, Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma 2003 na Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali ya Umma, 2005.

Ufisadi na utovu wa maadili ni mambo ambayo yanaathri vibaya ustawi wa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kitamaduni katika jamii yetu. Uchunguzi wa Mifano Mahsusi katika kitabu hiki unaonyesha baadhi ya athari hizi. Tunatarajia kuwa Wakenya watakaposoma kitabu hiki watachochewa kuchukua hatua mwafaka badala ya kufa moyo au kutojali kuhusu mambo ya ufisadi. Kwa hivyo, ni muhimu kwa watumishi wa umma, wananchi binafsi na umma kwa jumla kusoma mifano hii kisha waitumie kama mwongozo wa kutambua, kukabili na kuondoa kabisa uovu wa ufisadi katika nchi yetu hii tunayoipenda.

Prof. PLO - Lumumba, Ph.D
Mkurugenzi / Mtendaji Mkuu
Tume ya Kupambana na Ufisadi ya Kenya.

MFANO A

Chotara Mwenzangu ni mwanafunzi wa kigeni anayesoma kwenye chuo katika nchi moja jirani. Kwa kazi yake ya muhula, anafanya utafiti kuhusu uwezo wa jeshi la nchi ya Kenya kupambana na mashambulizi kutoka nchi zingine. Anahitaji habari zifuatazo kuhusu jeshi hili: muundo wa jeshi, idadi ya wanajeshi na vifaa vya vita walivyonavyo. Chotara anaitembelea idara ili aweze kupata habari hizi. Anapofika katika kiingilio cha idara anapata kibao kilichoandikwa maandishi haya **"HILI NI ENEO LISILOKUWA NA UFISADI."** Chini yake palikuwa na sanduku kubwa la mbao lililoandikwa: **"RIPOTI AINA YOYOTE YA UFISADI HAPA."**

Kerich Maarufu, mtumishi wa umma, ndiye anamhudumia anapowasili katika idara ya serikali. Baada ya kumsikiliza Chotara anamweleza kwamba idara yao hairuhusiwi kutoa habari kama hizi kwa umma kwa sababu zinahusu usalama wa taifa. Chotara anamsihi ampe majibu kwa sababu hawezi kufanya utafiti aliopewa chuoni bila habari hizi na huenda akalazimika kubadilisha mada yake ya utafiti, jambo ambalo hawezi kulifanya kwa kuwa tayari amechelewa kuwasilisha utafiti wake.

Kerich anaonekana kama kwamba anamhurumia Chotara kwa sababu ya shida aliyonayo. Anamwambia kwamba yuko tayari kumsaidia ikiwa atampa 'kitu kidogo' na pia amhakikishie kwamba hatafichua kuwa yeye ndiye aliyempa habari hizi. Anasisitiza kwamba iwapo itajulikana kuwa ndiye aliyempa habari hizi, basi atakuwa matatani sana. Chotara anamwahidi kwamba hatamwambia yeyote kuhusu jambo hili.

Kerich anamwambia Chotara aweke kiasi bainifu cha pesa katika bahasha. Anamweleza Chotara kwamba keshoye aje ikiwa ameificha bahasha hiyo ya pesa katikati mwa gazeti kisha ajifanye kana kwamba 'amesahau' gazeti hilo kwa meza yake. Chotara anakubali. Siku inayofuata, Chotara anawasili ofisini mwa Kerich akiwa na bahasha iliyofichwa ndani mwa gazeti. Kerich anampa hati zenye habari aliyohitaji kisha Chotara anatoka kwenye ofisi huku 'akisahau' gazeti lake juu ya meza ya Kerich.

Jioni hiyo, Chotara anapanda basi ili arudi nyumbani. Katika kituo cha mpakani, mkoba wake unakaguliwa na zile hati zinapatikana. Chotara anatiwa mbaroni na kuulizwa aeleze namna alivyozipata hati hizo. Anafichua kwamba alipewa hati hizo na Kerich alipomtembelea afisini mwake asubuhi ya siku hiyo. Siku inayofuata, polisi wanaenda katika ofisi ya Kerich na kumhoji, msimamizi wake akiwepo kuhusu namna Chotara alivyopata stakabadhi hizo. Kerich anakanusha madai haya kabisa kwa kusema kwamba hajawahi kumpa Chotara stakabadhi zozote. Anawaeleza polisi na msimamizi wake kwamba hana fununu yoyote kuhusu namna Chotara alivyopata stakabadhi hizo. Polisi wanaondoka na kumtaka aripoti kwenye kituo cha polisi siku hiyo baadaye ili waweze kumhoji zaidi.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) Hongo / Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kerich alimuuliza Chotara ampe 'kitu kidogo' ili ampe habari aliyohitaji. Kwa hivyo, anatenda uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti. Iwapo atapelekwa mahakamani, huenda atakabidhiwa na mashtaka ya uhalifu yafuatayo:

- Kuomba apewe hongo
- Kupokea hongo.

Chotara pia anatenda uhalifu wa kutoa hongo kwa maajenti.

b) Matumizi Mabaya ya Mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kerich alitumia mamlaka yake vibaya kwa kumnufaisha Chotara kwa kutoa habari za siri kinyume na sheria. Kerich alikuwa na habari hizi kwa mujibu wa mamlaka yake. Kutoa habari hizi za siri kwa mtu asiyeruhusiwa kuzipokea ni matumizi mabaya ya mamlaka.

c) Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 katika Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Kukiuka uaminifu hutokea wakati ambapo mtumishi wa umma, katika harakati ya kufanya kazi yake, anatenda mambo ya udanganyifu au kuufanya umma ukose uaminifu na utendakazi wake. Kerich alikuwa na mamlaka yanayohitaji uaminifu akiwa na jukumu la kutunza habari za siri. Ilimpasa asitoe habari hizi za siri. Kwa hivyo, kwa kutoa habari hizi, alivunja uaminifu.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Mamlaka ya Sheria- kifungu cha 10 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

Kerich anapaswa kufanya kazi yake kwa kuzingatia sheria. Kwa kutoa habari za siri bila ruhusa, Kerich alivunja Kanuni za Maadili. Kerich alienda kinyume na Sheria ya Siri Rasmi za Serikali.

b) Kutumikia Mtu wa Nchi ya Kigeni - kifungu cha 14 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

Kama mtumishi wa umma, Kerich anafaa kufanya kazi kwa namna ambayo haihatarishi usalama wa taifa la Kenya hasa anapotangamana na watu, mashirika au serikali za nchi za kigeni.

Kerich anavunja sheria hii wakati alipompatia mwanafunzi wa nchi ya kigeni habari zisizoruhusiwa kuhusu jeshi la nchi ya Kenya.

3. ***Je, ungelikuwa Kerich, ungefanya nini?***
4. ***Je, ungelikuwa Chotara, ungefanya nini?***
5. ***Ungelikuwa unafanya kazi na Kerich kisha ugundue alivyofanya, ungechukua hatua gani?***
6. ***Ungelikuwa msimamizi wa Kerich kisha makosa aliyoyafanya yaripotiwe kwako, ungechukua hatua gani ?***
7. ***Je, ungepata kujua jinsi mambo haya yalivyotokea, ungechukua hatua gani kama mwananchi?***

MFANO B

Mwanzoni mwa mwaka, gazeti moja la kila siku linatoa habari kwamba kuna upungufu wa walimu katika wilaya kadhaa nchini Kenya. Chapisho hilo linatoa fununu kwamba hivi karibuni kutakuwa na uajiri wa walimu utakaofanywa na Tume ya Kuwaajiri Walimu. Miezi kadhaa baadaye, Tume ya Kuwaajiri Walimu inatangaza kwenye magazeti kwamba walimu ambao wangependa kuomba kazi na wamehitimu, wanafaa kutuma barua za maombi ya kazi, tawasifu na stakabadhi zingine muhimu kwa afisi za elimu za wilaya ambako nafasi zimetangazwa.

Bi **Habibi Matatizo** anaposoma tangazo hili anakusanya stakabadhi zote zinazohitajika kwa haraka na kuzipeleka katika ofisi ya elimu katika wilaya yake. Habibi alihitimu mwaka wa 1999 kutoka chuo cha walimu cha *Mwalimu Bora Teachers Training College* lakini hajafanikiwa kupata kazi ya kudumu kufikia sasa.

Anapofika katika Ofisi ya Elimu, anaelekezwa kwa ofisi ya Bwana **Lukina Mporaji.** Huyu ni mmoja wa maafisa wa elimu katika wilaya hii. Lukina anamwambia Habibi kwamba amechelewa kuleta barua yake ya maombi kwa hivyo hatachukua stakabadhi zake. Habibi analalamika kuwa hajachelewa. Ili kuthibithisha kauli yake, anatoa mfukoni mwake gazeti ambalo lina tangazo hilo alilokuwa amelibeba mfukoni mwake kwa muda. Lukina anakataa kabisa kumsikiliza kisha anamwambia kwa madharau kwamba wamepata barua kutoka Tume ya Kuwaajiri Waalimu inayoonyesha kubadilishwa kwa tarehe ya kupokea barua za maombi ya kazi. Anamwambia Habibi aende na aache kupoteza wakati wake bure.

Bi. Almasi Msaidizi ambaye alisikia bila kukusudia yale waliyokuwa wakisema Habibi na Lukina, anampigia Lukina simu na kumwambia kwa sauti ya chini kwamba anayoyasema Habibi ni ya kweli. Almasi anauliza iwapo barua ilitumwa kwa ofisi zao ikionyesha kubadilishwa kwa siku ya kupokea barua za maombi; maanake yeye hajapata habari za kubadilishwa tarehe. Lukina anamwambia Almasi ashughulikie mambo yanayomhusu na awache kusikiliza mazungumzo yao. Almasi anakata simu kwa upole. Baada ya kulalamika kwa muda, sasa akilia machozi na kuelekea kufa moyo, Habibi anamuuliza Lukina ni nini atafanya ili barua yake iweze kuwekwa pamoja na zile zingine zilizoletwa awali. Anamwambia Lukina kwamba ametafuta kazi kwa muda mrefu na atakuwa na huzuni nyingi ikiwa atapoteza nafasi hii. Lukina akijifanya kuwa amepunguza ukali wake, anamwambia Habibi kwamba anaweza kumpa usaidizi kwa njia ya mapendeleo. Anamwambia kuwa yeye ndiye anasimamia upokeaji wa barua za maombi ya kazi na anaweza kuchukua barua yake kisha akaiweka pamoja na zile zilizoletwa awali bila mtu yeyote kujua. Hata hivyo, lazima Habibi awe tayari kumfaa kwa namna fulani.

Lukina anamwambia kuwa yeye ni msichana mrembo na angependa wajuane zaidi. Anamwomba Habibi wakutane siku hiyo jioni, ili wale chakula pamoja. Vilevile, anamwambia kwamba kujaliwa kwake kupata kazi, kutategemea jinsi atakavyoshirikiana naye kwa sababu ana cheo kikubwa

na anaweza kumsaidia kupata kazi yoyote anayotaka. Siyo lazima afuate mpangilio au utaratibu uliowekwa ambao ni mrefu ili apate kazi. Habibi hawezi kusitiri mshangao wake. Anapoendelea kuongea, Lukina anatembea hadi mahali Habibi alikuwa ameketi kisha anaweka mkono wake kwa mabega yake. Habibi anakasirishwa sana na jambo hili, anasimama kisha anasukuma mkono wa Lukina kutoka kwa mabega yake. Anaondoka ofisini humo akiwa amebeba barua yake ya maombi mkononi.

Maswali

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) Hongo / Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Hongo si lazima iwe pesa. Lukina alimwambia Habibi wakutane jioni ili aweze kumsaidia kupata kazi. Kwa hivyo, amevunja sheria inayohusu kutoa hongo inayowahusisha maajenti hata kama kitendo hakikutendeka, mradi tu aliomba hongo. Kwa hivyo, Lukina anatenda makosa ya kuomba hongo kwa njia ya kutaka kufanya mapenzi na Habibi.

b) Matumizi Mabaya ya Mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi.

Serikali inatarajia kuwa Lukina ambaye ni Ofisa wa Elimu wa Wilaya atafanya kazi kama mweledi yaani bila uoga au mapendeleo. Serikali pia inatarajia kwamba Lukina atakuwa na tabia ambayo itavutia umma kuwa na imani katika kazi yake. Anapomnyanyasa Habibi kimapenzi, hawezi kuaminika. Kwa hivyo, anafanya kosa la kutumia mamlaka yake vibaya.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Lukina anamnyanyasa Habibi kijinsia – kifungu cha 21 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kumnyanyasa mtu kijinsia kunahusu mambo yafuatayo:

i) Kumhitaji mtu ahusiane nawe kimapenzi;
ii) Kumshika mtu sehemu za mwili kimakusudi kwa njia inayoonyesha kuwa unataka kufanya mapenzi naye; au
iii) Kutoa matamko ya kijinsia kwa mtu fulani.

b) Utovu wa Utaalamu – kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma anatarajiwa kufanya kazi yake huku akizingatia sheria na taratibu zilizopo. Zaidi ya hayo, kila mtumishi wa umma aliyeajiriwa na serikali anafaa kuzingatia Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma, 2003 ambayo inaeleza tabia ambayo kila afisa anafaa kuonyesha. Unaweza sasa kutumia Sheria hii kujua uwajibikaji wa mtumishi wa umma kutokana na mambo anayotenda au anayokosa kuyatenda. Lukina alionyesha kiburi, utovu wa adabu na heshima sio tu kwa Habibi bali pia kwa Almasi ambaye ni mfanyikazi mwenzake.

c) Kupeana habari za uongo na zinazopotosha - kifungu cha 19 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Lukina anamdanganya Habibi kuhusu siku ya mwisho ya kupokea barua za maombi ya kazi.

d) Kuchagua mtumishi wa umma bila kuzingatia uaminifu, utendakazi na kuhitimu kwake - kifungu cha 22 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Lukina anataka kumsaidia Habibi apate kazi bila kuzingatia kuhitimu au kufuzu kwake kitaalamu.

3. Je, ungekuwa Habibi, ungefanya nini?

4. Je, ungekuwa Almasi, ungechukua hatua zipi?

5. Kama ungekuwa msimamizi wa Lukina, kisha makosa aliyoyafanya yaripotiwe kwako, ungechukua hatua gani?

MFANO C

Chweya Biashara ameajiriwa kama daktari katika Hospitali ya Wilaya. Pia ana kliniki yake mjini anakotekelezea shughuli zake nyingi. Amewaachia wauguzi katika Hospitali ya Wilaya maagizo makali kwamba mgonjwa yeyote anayemtaka au angetaka ushauri wake, aende katika kliniki yake mjini. Hata hivyo, licha ya kuwa hapatikani katika Hospitali ya Wilaya, Chweya anaendelea kupokea mshahara kila mwisho wa mwezi kutoka kwa serikali, hata kwa siku zile ambazo hawahudumii wagonjwa hospitalini.

Hivi karibuni kliniki ya Chweya imepungukiwa na wateja. Hali hii imempelekea kuwa na madeni mengi huku wadeni wake wakimtafuta ili awalipe pesa zao. Wiki chache zilizopita, mmoja wa wadeni hawa alimtuma dalali ambaye alifunga kliniki na akatwaa mali ya Chweya ili kulipia kodi ya nyumba aliyokuwa ameshindwa kulipa kwa muda na kisha akafunga kliniki hiyo. Mnada wa kuuza mali hiyo unatarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Wadeni wengine wamepata fununu kuhusu mnada utakaofanywa na wanamtafuta Chweya ili awalipe. Chweya ameenda mafichoni. Haendi kazini na hapatikani nyumbani kwake. **Msimamizi wa Madaktari** katika hospitali ya wilaya amekuwa na wakati mgumu kwa sababu wanaomdai Chweya pesa walienda kumuona wakitaka kujua aliko. Wanaofanya kazi naye, ambao wamekutana na Chweya kisadfa, wanasema kuwa Chweya ni mchafu na anakunywa pombe kupindukia.

Msimamizi wa Madaktari ameandika barua kwa makao makuu ya Wizara ya Afya akipendekeza Chweya aachishwe kazi mara moja kwa sababu amekosekana kazini kwa muda mrefu. Hata hivyo, siku chache baadaye, Chweya anamtembelea Msimamizi wa Madaktari nyumbani kwake, akimsihi amsaidie ili asipoteze kazi. Anaahidi kuwa atarejea kazini mara moja kisha anampa bahasha iliyo na shilingi elfu 30,000 kama ‘zawadi’ kwa familia yake.

Msimamizi wa Madaktari anamshukuru Chweya kwa ‘zawadi’ aliyompa kisha anamwarifu kuwa tayari alikuwa amependekeza kwa Wizara ya Afya ili Chweya afutwe kazi. Kwa hivyo, anahitaji pesa zaidi kutoka kwake, ili ampe yule atakayetoa barua hiyo kutoka kwa faili yake. Chweya anakubali kuleta pesa hizo za ziada keshoye ili zipelekwe kwa makao makuu ya Wizara ya Afya na zipokezwe kwa yule atakayetoa barua kwenye faili. Chweya anamletea Msimamizi wa Madaktari pesa jinsi walivyoagizana, kisha anazituma kwa Kiburi Mzalendo, karani katika Ofisi ya Usajili. Anampa maagizo kuing’oa ile barua aliyokuwa ameiandika kisha aichane. Kiburi anapokea pesa kisha anaing’oa barua kwenye faili na kuichana kama aliivyoagizwa.

Maswali:

1.Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) Hongo / Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Chweya amefanya uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti. Uhalifu huu unahusu au inajumulisha makosa matatu:

- Kuahidi kutoa hongo: Alimletea Msimamizi wa Madaktari 'zawadi' ya shilingi elfu 30,000 ili aweze kumsaidia asifutwe kazi.
- Kutoa hongo: Alimpatia Msimamizi wa Madktari 'zawadi' ya shilingi elfu 30,000 ili amsaidie asifutwe kazi
- Kukubali kutoa hongo: Chweya alikubali kukabidhi pesa za ziada kwa Msimamizi wa Madaktari ili amtumie Kiburi kama hongo.

Msimamizi wa Madaktari pia amevunja sheria inayohusu hongo inayowahusisha maajenti. Uhalifu huu unahusu au unajumuisha makosa manne:

- Kupokea hongo: Msimamizi wa Madaktari kwa hakika alipokea shilingi elfu 30,000.
- Kuitisha hongo: Msimamizi wa Madaktari alimuomba Chweya amukabidhi pesa za ziada ili wamhonge Kiburi.
- Kuahidi kutoa hongo. Msimamizi wa Madaktari aliahidi kumpa Kiburi hongo katika makao makuu ya Wizara ya Afya.
- Kutoa hongo: Msimamizi wa Madaktari kwa hakika alimkabidhi Kiburi Mzalendo hongo.

Kiburi amefanya uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti. Uhalifu huu una kosa moja:

- Kupokea hongo: Kiburi alipokea hongo kutoka kwa Msimamizi wa Madaktari ili atoe barua iliyokuwa kwa faili ya Chweya katika Makao Makuu ya Wizara.

b) Matumizi Mabaya ya Mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Msimamizi wa Madaktari alitumia mamlaka yake vibaya alipompatia Chweya usaidizi. Alimfanya mtumishi wa umma, ambaye anafanya kazi katika Makao Makuu ya Wizara ya Afya atoe barua kwa faili ya Chweya. Kwa hivyo, anatumia mamlaka yake vibaya. Kiburi pia anatumia mamlaka yake vibaya anapotoa barua kwa faili ya Chweya.

c) Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Msimamizi wa Madaktari na Kiburi wamefanya kosa la kuvunja imani. Wao wamepewa jukumu na serikali la kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, ukweli na pia kuwa waaminifu. Wanaposhirikiana kutoa barua katika faili ya Chweya, wamevunja imani hiyo.

d)Kumdanganya mwajiri– kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Chweya, Kiburi na Msimamizi wa Madaktari wamefanya kosa la kudanganya mwajiri wao ambaye ni serikali. Chweya alitoa hongo ili Msimamizi wa Madaktari aiondoe barua aliyokuwa ameandika akiripoti kutofika kazini. Msimamizi wa Madaktari alikula njama na Kiburi kisha wakang'oa barua hiyo kwenye faili. Ikiwa serikali itaangalia faili ya Chweya, baada ya barua hiyo kutolewa, itaonekana kuwa Chweya amekuwa akiripoti kazini na kufanya kazi huku akizingatia kanuni zinazokubalika kazini. Kwa hivyo, Serikali itaendelea kumlipa mshahara. Chweya, Msimamizi wa Madaktari na Kiburi wamedanganya serikali kiasi cha kuwasababishia wananchi wa Kenya hasara.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka.

Chweya, Kiburi na Msimamizi wa Madaktari wamekiuka Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma, 2003. Ukiukaji huu ni pamoja na:

a) Kujitajirisha kwa kutumia mbinu zisizofaa – kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Msimamizi wa Madaktari amekiuka sheria ya maadili anapopokea 'zawadi' ya shilingi 30,000 kutoka kwa Chweya. Anajua dhahiri shahiri au anapaswa kujua kwamba hafai kupokea zile pesa kwa sababu Chweya anatarajia kunufaika na uamuzi wa kutoadhibiwa.

b) Kuendesha shughuli za kibinafsi – kifungu cha 20 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma inasema kwamba inafaa mtumishi wa umma afanye shuguli zake za kibinafsi kwa namna ambayo itahifadhi imani ya umma kwa uadilifu wa afisi yake. Aidha, mtumishi wa umma anafaa kutimiza majukumu yake ya kifedha bila ya kuyapuuza. Chweya anafanya makosa anapopuuza au kukataa kulipa wanaomdai na badala yake akaamua kujificha ili wasimpate.

c) Mgongano wa Maslahi – kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Si vibaya Chweya kuwa na kliniki ya kibinafsi lakini kuna uwezekano wa kugongana kwa maslahi kwa kuwa yeye ni dakatari wa serikali. Hata hivyo, majukumu yake yanaweza kuhitilafiana wakati anapofanya kazi kama daktari katika kliniki yake na wakati huo huo kuwa Daktari wa Hospitali ya Wilaya.

3. Je, ungekuwa Msimamizi wa Madaktari katika hospitali ya wilaya, ungechukua hatua zipi?

4. Je, ungekuwa Kiburi Mzalendo, ungefanya nini?

5. Ikiwa wewe ni mwananchi kisha uelezewe kuhusu mambo haya, ungefanya nini?

MFANO D

Mjuaji Marco ni Katibu wa Mji wa ***Tuendelee Municipal Council.*** Hivi majuzi, ameanzisha biashara mjini inayojulikana kama ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers.*** Biashara hii inahusu vifaa vya kuandikia.

Tuendelee Municipal Council wametangaza zabuni (tangazo linalotoa habari au kualika maombi ya watu wanaotaka huduma pamoja na kutoa gharama za huduma hizo) ya shilingi 300,000/- ili waletewe vifaa vya kuandikia. ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers*** na kampuni nyingine za biashara wanaomba kupewa zabuni hii. Mjuaji Marco kwa kutumia mamlaka yake kama Katibu wa Mji anamuamrisha Mtiifu Paulo, mfanyakazi wa baraza la Mji anayejua mahali kunakowekwa ufunguo wa kijisanduku cha zabuni, afungue kijisanduku hicho, kisha amwambie kiasi cha pesa kilichotajwa kwa gharama hiyo na wawaniaji wengine. Anapofungua kijisanduku hicho anagundua kwamba ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers*** wametaja bei ya juu kuliko kampuni nyinginezo, na kwa sababu hiyo huenda wasipate zabuni hiyo. Mjuaji anayaondoa maombi ya zabuni ya ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers*** na kuyabadilisha na maombi mapya yanayotaja bei ya chini zaidi kuliko kampuni nyinginezo.

Katika mkutano wa kamati inayoshughulikia zabuni hii, Mjuaji hatangazi kuegemea kwake kwa kampuni ya ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers***. Anashiriki katika mikutano ya kamati inayojadili zabuni hii na anakubaliana nao kwamba ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers*** wapewe zabuni hiyo.

Mlanawe Yohana, mtumishi wa umma ambaye anasimamia uidhinishaji wa bidhaa katika ***Tuendelee Municipal Council*** anapokea vifaa vya kuandikia kutoka kwa ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers***. Anapochunguza bidhaa hizo anagundua kwamba bidhaa hizo zina kasoro na hazitimii kiwango kilichoagizwa. Anatishia kukataa bidhaa hizo zote.

Mporaji Maarufu ambaye ni muuzaji kutoka ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers*** anamsihi **Mlanawe** asikatae bidhaa zao. Anamwambia Mlanawe kwamba ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers*** ni kampuni inayomilikiwa na Katibu wa Mji na watampa 'zawadi nono' ikiwa atakubali bidhaa zao kama zilivyo. **Mporaji**, anatoa kibunda cha noti za shilingi elfu moja moja na kukiweka mikononi mwa **Mlanawe** ili amuamini. **Mlanawe** anaziweka pesa hizi mfukoni mwake kisha anathibitisha kuwa amepokea bidhaa hizo. Baada ya hayo, Mjuaji anahakikisha ***Bidhaa za Kushangaza Suppliers*** wanalipwa haraka haraka bila kufuata utaratibu unaofaa.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa na watu katika hadithi hii. Aina hizi ni pamoja na:

a) Mjuaji Marco ametenda uhalifu ufuatao:

- **Mgongano wa Maslahi – kifungu cha 42 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Mjuaji alitaka apewe zabuni kwa sababu Bidhaa za Kushangaza Suppliers ni kampuni yake na pia kwa kuwa yeye ni Katibu wa Mji wa ***Tuendelee Municipal Council***. Hakutangaza ukweli huu na badala yake akahusika katika kamati iliyofanya uamuzi wa nani atapewa zabuni.

- **Ulaghai katika uwaniaji wa zabuni – kifungu cha 44 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Mjuaji alimuamrisha Mtiifu Paulo afungue kijisanduku cha zabuni usiku kisha amwambie kuhusu zabuni za kampuni zingine pinzani. Kisha alichukua zabuni ya kwanza iliyokuwa imeandikwa na Bidhaa za Kushangaza Suppliers, akaibadilisha na ya pili iliyotaja gharama ya chini mno kuliko kampuni pinzani.

- **Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Mjuaji alitumia mamlaka yake vibaya kwa sababu alitumia njia isiyo halali na yenye hila ili kampuni yake ipate zabuni.

- **Kukiuka Uaminifu– kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu (Penal Code)**

  Mjuaji amekiuka misingi ya uaminifu kwa sababu Baraza la Mji linamtarajia afanye kazi kwa kuzingatia uaminifu na ustadi. Hakutangaza kuwa anaijua kampuni iliyopewa zabuni na ambayo inawasilisha bidhaa zenye kasoro na za idadi isiyotimia viwango vilivyoagizwa.

- **Uhalifu wa kiuchumi – kifungu cha 45 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Mjuaji ndiye amechangia pakubwa Bidhaa za Kushangaza Suppliers kulipwa licha ya bidhaa zao kuwa zenye kasoro na kupungua idadi ya viwango vilivyoagizwa. Alihakikisha kuwa wamelipwa kwa haraka bila kuzingatia taratibu zinazofwatwa na Baraza la Mji.

b) Mlanawe Yohana ametenda uhalifu ufuatao:

- **Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti - kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Mlanawe amehongwa na Mporaji ili apokee bidhaa kutoka Bidhaa za Kushangaza Suppliers licha ya kuwa bidhaa hizo zilikuwa na kasoro. Kwa hivyo, anafanya kosa la hongo inayowahusisha maajenti.

- **Kumdanganya Mwajiri – kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**
  Mlanawe alitia sahihi kuthibitisha kuwa bidhaa alizopokea zilitimiza idadi na viwango vilivyohitajika na Baraza la Mji na hivyo basi, Baraza la Mji likalipa Bidhaa za Kushangaza Suppliers. Mlanawe alimdanganya muajiri wake.

- **Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**
  Mlanawe alitumia mamlaka yake vibaya alipokubali kupokea bidhaa ambazo bali na kuwa na kasoro hazikutimia idadi iliyoagizwa. Vilevile, alitumia mamlaka yake vibaya kwa kupokea hongo kutoka kwa Bidhaa za Kushangaza Suppliers.

- **Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu (Penal Code)**
  Mlanawe alikiuka imani kwa sababu Baraza la Mji linamtarajia afanye kazi kwa kuzingatia uaminifu na ufanisi. Hata hivyo, alikubali kupokea bidhaa ambazo zina kasoro na zisizotimia idadi iliyoagizwa.

- **Uhalifu wa kiuchumi – kifungu cha 45 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**
  Mlanawe alihusika katika kosa la uhalifu wa kiuchumi. Alipokea bidhaa ambazo alijua kuwa zina kasoro na zisizotimia idadi iliyoagizwa. Bidhaa za Kushangaza walilipwa baada ya Mlanawe kuidhinisha kuwa bidhaa alizopokea zilitimia idadi iliyoagazwa ilhali yote haya ni kinyume cha hali halisi. Mlanawe anatenda makosa mawili kwa:
  1. Kupokea bidhaa za dhamani duni
  2. Kupokea bidhaa zisizotimia kiasi kilichoagizwa

c) Mporaji Maarufu ametenda uhalifu ufuatao:

- **Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti - kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**
  Mporaji alimhonga Mlanawe ili akubali bidhaa zao ambazo bali na kuwa na kasoro zilipungua viwango vilivyoagizwa na Baraza la Mji. Anatenda uhalifu wa kutoa hongo.

d) Mtiifu Paulo anatenda uhalifu ufuatao:

- **Ulaghai katika uwaniaji wa zabuni – kifungu cha 44 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**
  Mtiifu Paulo alifungua kijisanduku cha zabuni usiku kisha akamwambia Mjuaji kuhusu kiwango cha pesa kilichotajwa na kampuni pinzani. Kwa hivyo alitenda uhalifu wa ulaghai katika uwaniaji wa zabuni.

- **Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Mtiifu alijua mahali panapowekwa ufunguo wa kijisanduku cha zabuni. Alitumia mamlaka yake vibaya wakati alipofungua kijisanduku hicho na kumdokezea Mjuaji habari kuhusu zabuni zilizoletwa na kampuni pinzani.

- **Kukiuka uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu**

Baraza la Mji limempa Mtiifu jukumu la kufanya kazi na linatarajia kwamba atafanya kazi yake kwa uaminifu na uwajibikaji. Alivunja sheria alipohusika katika matendo ya udanganyifu.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

- **Mamlaka ya Sheria – kifungu cha 10 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**

  Kulingana na Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma, 2003; Mjuaji, Mtiifu na Mlanawe wanapaswa kuheshimu mamlaka ya sheria katika utendakazi wao. Walikosa kufanya hivyo kwa njia zifuatazo:

  i) Mjuaji hakutangaza kwa uwazi mgongano wa maslahi uliokuweko.

  ii) Mtiifu alimpa Mjuaji habari ambazo hakustahili apewe na hivyo kumnufaisha.

  iii) Mlanawe alipokea idadi ndogo isiyotimia viwango vilivyoagizwa na pia aliamrisha Bidhaa za Kushangaza Suppliers ilipwe licha ya bidhaa zao kuwa na dhamani duni.

- **Mgongano wa maslahi– kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**

  Kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma, 2003 kiinaeleza kuwa mtumishi wa umma anafaa kuhakikisha kuwa shughuli zake za kibinafsi hazihitilafiani na kazi yake rasmi. Pia kifungu hiki kinaelezea kuwa mtumishi wa umma hafai kutoa kandarasi au kushawishi wanaohusika kutoa kandarasi ili kujiletea faida yeye mwenyewe, bibi yake, mshirika wake wa biashara, kampuni anayoshirikiana nayo kibiashara au shirika lolote lile analohusiana nalo kibiashara. Mjuaji alitenda uhalifu huu alipokosa kutangazia kamati kuwa Bidhaa za Kushangaza Suppliers inayoomba zabuni ni biashara yake mwenyewe.

3. Je ungelikuwa Mlanawe, ungelifanya nini?

4. Je, ungelikuwa Mtiifu Paulo, ungelifanya nini?

5. Kama ungekuwa mfanyikazi mwenzi wa Mlanawe kisha baadaye upate kusikia yale yaliyotendeka, ungelifanya nini?

6. Kama ungekuwa msimamizi wa Mlanawe kisha mambo haya yaripotiwe kwako, ungechukua hatua gani?

7. Kama ungekuwa mwananchi ambaye anajua yale yaliyotendeka, ungechukua hatua gani?

MFANO E

James Mabadiliko ni mwanzilishi na mwanachama wa Tudumishe Uzalendo, shirika ambalo si la kiserikali lenye nia ya kukuza uzalendo nchini Kenya. Shirika hili linahimiza ukuzaji wa uzalendo kama njia ya kimsingi mwafaka ya kupambana na ufisadi na kuimarisha usalama hapa nchini. Shirika hili limeajiri zaidi ya watu kumi na watano (15) na hupata msaada kutoka kwa wahisani unaosaidia kuendeleza kazi zao. Baadhi ya msaada waliopokea umetumika kununua magari ili waweze kuwatembelea wananchi kuandaa warsha mashinani.

Hivi karibuni, James ameanzisha biashara ya kukarabati magari inayoitwa **Jua Kali Auto Garage**. Anaona kuwa shirika hili litailetea gereji yake biashara. Anamwendea **Wemasa Mapambano,** Mkurungezi Mkuu wa Shirika la Tudumishe Uzalendo, na kumpendekezea kwamba 'amsaidie' ili magari ya shirika lake yawe yakikarabatiwa katika gereji yake. James anamwahidi Wemasa kuwa yuko tayari kumpa asimilia fulani ya malipo yoyote atakayopata. Wemasa anakubali pendekezo hili mara moja.

Muda mfupi baadaye, Kamati ya Fedha ya shirika hili inatangaza zabuni ya kukarabati magari ya shirika hili. Kamati hii inatoa masharti yatakayozingatiwa ili gereji ipate zabuni. Gereji zinazoomba zabuni hazifai kutajiwa masharti haya. Wemasa kama Mkurugenzi Mtendaji ni mwanakamati wa kamati inayohusika kupeana zabuni. Wapokamilisha mkutano, Wemasa anampigia James simu na kisha kumwarifu masharti yatakayozingatiwa ili gereji yao ipate zabuni. Jua Kali Auto Garage inapeleka maombi ya zabuni yake huku ikizingatia masharti haya.

Kamati ya Fedha inapokutana kujadiliana na kutoa uamuzi kuhusu zabuni, Wemasa hafichui kuwa ana maslahi fulani katika zabuni hiyo. Isitoshe, anashiriki katika majadiliano na maamuzi kuhusu gereji ipi inafaa kupewa zabuni. **Jua Kali Auto Garage** inapewa zabuni hii ya kukarabati magari.

Kupitia uamuzi huu, shirika la **Tudumishe Uzalendo** linatuma magari yao kwa gereji ya **Jua Kali Auto Garage** ili yakarabatiwe. Gereji hii haina uwezo wa kiufundi unaohitajika na wanayaharibu magari zaidi badala ya kuyatengeneza. Isitoshe, makanika wa gereji hii huviondoa vipuri vipya kutoka kwa magari haya na kuvibadilisha na vipuri vikuukuu. Kisha wanaviuza vipuri hivyo vipya.

Hali mbaya ya magari ya shirika, baada ya kukarabatiwa inamfanya **Amali Mwangalifu,** ambaye ni msimamizi wa shirika la **Tudumishe Uzalendo**, kumlalamikia Wemasa kuhusu ukarabati mbaya unaofanywa na gereji hii. Wemasa anamhakikishia kwamba atachunguza mambo haya. Hata hivyo, hafanyi chochote.

Inapofika mwisho wa mwezi, **Jua Kali Auto Garage** wanadai malipo ya juu kuzidi viwango vilivyowekwa wakati wa kupewa zabuni. Baadhi ya sababu wanazotoa kwa kuongeza bei yao ni kwamba gharama ya maisha imepanda.

Amali anamlalamikia Wemasa kuhusu jambo hili na kumshauri asiwalipe kwa sababu hali ya magari yao imezorota zaidi ikilinganishwa na jinsi ilivyokuwa hapo awali na pia jumla ya pesa wanazodai haziambatani na mktaba uliowekwa. Wemasa anatupilia mbali mashauri ya Amali na kuidhinishwa walipwe. Kwa hivyo Jua Kali Auto Garage wanalipwa pesa zao. Baadaye, Wemasa anapokea asilimia ya malipo haya kama zawadi.

Amali anamwarifu Wemasa kuwa atazua swala la mkataba wa Jua Kali Auto Garage katika mikutano ya Bodi inayosimamia shirika la Tudumishe Uzalendo. Vilevile, anamueleza kuwa huenda akataja haya yaliyotendeka katika ripoti atakayoandikia wafadhili. Kwa kiburi, Wemasa anamwambia Amali kuwa yeye ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo na anaweza kufanya lolote atalotaka. Kwa dhihaka, anamwambia Amali kwamba anaweza kumripoti kwa ofisi yoyote anayotaka. Halafu anamfuta kazi Amali na kumuamrisha atoke katika ofisi za shirika mara moja. Anatoa agizo kwa walinda usalama wa shirika hilo wasiimruhusu Amali mahali popote karibu na ofisi za shirika hilo.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

- **Hongo / Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  James alimuahidi Wemasa asilimia fulani ya pesa zote ambazo Jua Kali Auto Garage angelipwa ili kumshawishi Wemasa awape **Jua Kali Auto Garage** zabuni. Kwa kufanya hivyo, anatenda uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti na kwa hivyo ana hatia zifuatazo:

  - Kuahidi kutoa hongo
  - Kutoa hongo

  Wemasa pia anatenda uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti. Alikubali kusaidia Jua Kali Auto Garage kupata zabuni ili naye anufaike kwa asimilia fulani ya malipo kwa gereji hiyo. Kwa hivyo, ana hatia ya kupokea hongo.

- **Mgongano wa maslahi - kifungu cha 42 cha cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Wemasa hakuitangazia Kamati ya Fedha iliyojadiliana na kutoa uamuzi kuhusu zabuni kuwa alikuwa na maslahi katika zabuni hiyo. Kwa hivyo, ana hatia ya mgongana wa maslahi.

- **Ulaghai katika uwaniaji wa zabuni - kifungu cha 44 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi.**

  Wemasa alimpa James habari zilizobanwa ambazo hazikutakikana kujulikana kwa waomba zabuni. Kwa kupokea hizi habari, James alinufaika visivyo. Kwa hivyo, James aliweza kutayarisha maombi yake ya zabuni akijua bayana masharti ya siri yaliyohitaji kuzingatiwa

na kamati amuzi. James na Wemasa wamefanya ulaghai katika uwaniaji wa zabuni.

- **Matumizi mabaya ya mamlaka –kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Matumizi mabaya ya mamlaka hujitokeza pale ambapo mtumishi wa umma anatumia mamlaka yake ili kujinufaisha au kuwanufaisha wengine kwa njia isiyo halali. Katika tukio hili, Wemasa alitumia mamlaka yake vibaya kwa sababu alisaidia Jua Kali Auto Garage kwa njia isiyo halali ili wapate zabuni. Cheo chake Wemasa kilimuwezesha kujua masharti ambayo yanazingatiwa na kamati. Anatoa masharti haya kwa ***Jua Kali Auto Garage*** ili aweze kujinufaisha.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Ingawa mashirika yasiyo ya kiserikali na wafanya kazi wao hawahusishwi katika Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma, 2003, ukiukaji wa maadili ulioelezwa katika tukio hili unafaa kuchunguzwa kuambatana na Kanuni Mahsusi za Maadili Mema zinazotumika kwa shirika lisilo la kiserikali linalohusika.

3. Je, ungelikuwa Wemasa, ungelifanya nini?

4. Je, ungelikuwa Amali, ungelifanya nini?

5. Kama ungekuwa unafanya kazi na Amali kisha baadaye ujue yaliyotendeka, ungechukua hatua gani?

6. Kama ungekuwa mwanakamati wa Bodi ya Tudumishe Uzalendo kisha matukio haya yaripotiwe kwako, ungechukua hatua gani?

7. Kama ungekuwa ni mwananchi ambaye ameshuhudia yaliyotendeka, ungechukua hatua gani?

MFANO F

Inashukiwa kwamba kiwanda cha ***Mkono Gamu Factory*** kilipatikana kupitia kwa ufisadi. Wakurugenzi wa kiwanda hiki wamepewa notisi na wapelelezi ili waeleze jinsi walivyopata kumiliki ***Mkono Gamu Factory.*** Huku wakiendelea na upelelezi, wapelelezi wanataka mahakama iteue Meneja-Mrasimu wa Mkono **Gamu Factory**, kwa sababu kuna wasiwasi jinsi kiwanda hiki kinavyoendeshwa na hakijaonyesha dalili za kufilisika.

Kinio Maliza, anaposikia kwamba wapelelezi wanataka mahakama iteue Meneja-Mrasimu, anaenda kumuona anayeongoza upelelezi, Ian Msimamizi ili ateuliwe kama Meneja-Mrasimu. Ian anapendekeza Kinio ateuliwe. Kwa hivyo, mahakama inamteua Kinio kama Meneja-Mrasimu.

Kabla ya uteuzi huu **Kinio Maliza** alimwahidi Msimamizi 'zawadi kubwa'. Msimamizi naye hakuiambia mahakama au wapelelezi chochote kuhusu ahadi hiyo ya 'zawadi kubwa.' Baada ya kuteuliwa, Kinio anampelekea Ian gari jipya aina ya ***'S-class Mercedes Benz.'***

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna ufisadi wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

- **Manufaa yasiyofaa kwa mdhamana ili kuteuliwa – kifungu cha 43 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Uteuzi wa Kinio Maliza kama Meneja-Mrasimu wa Mkono Gamu Fatory utamuwezesha kuwa mdhamini wa mahakama, wapelelezi na mtu mwingine yeyote atakayefaidika kutoka kwa kiwanda hiki. Kinio alimwahidi Ian, kiongozi wa wapelelezi, zawadi kisha baadaye akampa zawadi hiyo ili mahakama iweze kumteua kama Meneja-Mrasimu. Zawadi hii ilikuwa siri kati ya Kinio na Ian. Kwa hivyo, wote wana hatia inayohusiana na manufaa yasiyofaa kwa mdhamana ili kuteuliwa.
- **Vishawishi vya kisiri kuhusu ushauri – kifungu cha 40 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

  Ian Msimamizi, kama kiongozi wa upelelezi, ana jukumu la kushauri Mamlaka ya Upelelezi na mahakama. Halmashauri hutegemea ushauri wake ili kufanya uamuzi wa aina mbali mbali. Maliza alimwendea Msimamizi akamuomba ashauri mahakama imteue kama Meneja-Mrasimu wa Mkono Gamu Factory. Maliza anamwahidi msimamizi kisiri kuwa akimsaidia atamletea 'zawadi kubwa.' Msimamizi na Maliza wote wana hatia ya kufanya vishawishi vya kisiri kuhusu ushauri.

- **Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**
  Kinio alimwahidi Ian Msimamizi 'zawadi kubwa' ikiwa atatoa pendekezo kwa mahakama kuwa ateuliwe kuwa Meneja-Mrasimu wa kiwanda cha Mkono Gamu Factory. Baada ya kuteuliwa anamletea Ian gari jipya aina ya 'Mercedez Benz'. Ian na Kinio wanatenda uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti.

  Maliza ana hatia ya kupeana hongo.

  Msimamizi ana hatia ya kupokea hongo.

- **Matumizi mabaya ya mamlaka – Kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**
  Ian Msimamizi anatumia mamlaka yake vibaya anapopendekeza **Kinio Maliza** ateuliwe kama Meneja-Mrasimu wa ***Mkono Gamu Factory*** kisha naye apate 'zawadi kubwa' ambayo ni gari jipya aina ya ***'S-class Mercedez Benz'***.

- **Kukiuka Uaminifu – Kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu (Penal Code)**
  Ian alifanya uhalifu wa kuvunja imani. Mamlaka ya Upelelezi iliamini kuwa Ian atawashauri kwa njia ya uaminifu na ukweli. Lakini **Ian Msimamizi** hakufanya hivyo.

2. ***Je, ungelikuwa Ian, ungelifanya nini?***
3. ***Kama ungekuwa mwananchi kisha ujue yale yaliyofanywa na Msimamizi na Maliza, ungechukua hatua gani?***

MFANO G

Mzee Wamafua aliishi mtaa wa Matajiri katika mji wa Wazalendo. Alikuwa mzee tajiri sana na alimiliki basi nyingi zilizoenda mashambani, malori kadhaa, maduka na nyumba za kukodisha. Vilevile, alimiliki hekta nyingi za ardhi kule Malezi ambako alipanda maua, ndizi na machungwa ambayo aliuza kule Uropa.

Takriban mwezi mmoja uliopita, Mzee Wamafua alipatwa na mshtuko wa moyo kisha akafariki. Baada ya kumzika, iligunduliwa kuwa Mzee Wamafua hakuacha wasia. Jambo hili lilileta shida kwa sababu alikuwa na bibi watatu na watoto ambao walianza kung'ang'ania mali yake. Kabla ya muda usio mrefu kupita, tatizo hili lililetwa mbele ya mahakama, ili mahakama iamue. Mahakama ikamchagua Mdhamini wa Umma kama msimamizi wa mali ya Mzee Wamafua.

Albero Mlaji, mmoja wa wanasheria katika ofisi ya Mdhamini wa Umma, alienda kumwona msimamizi wake, **Barafu Obadiah** akiwa na pendekezo kwamba angependa achaguliwe kusimamia kesi ya Mzee Wamafua . Albero ana hakika kuwa atafaidika kutoka kwa mali ya Mzee Wamafua. Obadiah anamuuliza Mlaji ampe muda ili afikirie kuhusu ombi lake.

Keshoye asubuhi, Albero anaenda kwa ofisi ya Obadiah akiwa na bahasha mkononi. Albero, kwa kuwa anajua kwamba Barafu amekuwa akichangisha pesa za kumpeleka mwanawe ng'ambo kusoma, anamletea shilingi 30,000/- ndani ya bahasha kama mchango wake 'mdogo'. Obadiah anapokea bahasha hii kwa furaha kisha anampatia Albero kesi ya Mzee Wamafua ili ashughulikie. Familia ya Mzee Wamafua haiambiwi chochote kuhusu mchango uliotolewa na Mlaji.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna ufisadi wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) **Manufaa yasiyofaa kwa mdhamana ili kuteuliwa – kifungu cha 43 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Albero alimpatia Obadiah 'mchango mdogo' kwa ajili ya harambee ya mwanawe. Anafanya hivi ili Obadiah ampe kesi ya Mzee Wamafua ashughulikie. Familia ya Mzee Wamafua haijui lolote kuhusu 'mchango mdogo' ambao Obadiah alipokea. Kwa hivyo Mlaji na Obadiah wanafanya kosa la kutumia udanganyifu kumchagua Mdhamana atakayesimamia mali ya Mzee Wamafua.

b) Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Mlaji alimpa Obadiah shilingi 30,000/- kama 'mchango mdogo' kwa harambee ya kuchangia mvulana wake pesa. Mchango huu ulitolewa kumsinikiza Barafu aweze kumpa Albero kesi ya Mzee Wamafua ashughulikie. Mlaji na Obadiah wanatenda uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti.

Mlaji anatenda uhalifu wa kutoa hongo.

Obadiah anatenda uhalifu wa kupokea hongo.

c) Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Obadiah alitumia mamlaka yake vibaya wakati alipompatia Albero Mlaji ashugulikie kesi ya Mzee Wamafua kwa sababu alimletea shilingi 30,000/- kama mchango wa harambee ya mvulana wake.

2. ***Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?***

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Kujitajirisha kwa kutumia mbinu zisizofaa – kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma kinaeleza kuwa hakuna mtumishi wa umma anayeruhusiwa kuitisha au kupokea zawadi au fadhila kutoka kwa mtu anayetaka huduma fulani. Obadiah alipokea shilingi 30,000/- kutoka kwa Albero ambaye alitaka ashughulikie kesi ya Mzee Wamafua. Kwa hivyo, anavunja Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

b) Michango na Harambee – kifungu cha 13 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

Kifungu cha 13 cha sheria ya Maadili ya Mtumishi wa Umma kinaeleza kuwa mtumishi wa umma hatatumia afisi yake au mahali pake pa kazi kuwa mahali pa kuomba au kuitisha mchango.

Obadiah alivunja sheria hii kwa kupokea shillingi 30,000/- kutoka kwa Albero kama mchango wa harambee ya mvulana wake.

3. ***Je, ungelikuwa Obadiah, ungelifanya nini?***
4. ***Je, ungelikuwa mmojawao wa familia ya Mzee Wamafua, kisha upate kujua kwamba Obadiah alipatiwa 'zawadi' ili ampe Albero Mlaji kesi ya Wamafua aishugulikie, ungelifanya nini?***
5. ***Kama ungekuwa mwananchi kisha baadaye upate kujua kuhusu mpango waliofanya Mlaji na Obadiah, ungechukua hatua gani?***

MFANO H

Kamau Mkarimu ni Afisa Mtumishi Mkuu katika Idara ya Mifugo ambayo iko chini ya Wizara ya Ustawi wa Mifugo na Uvuvi. Hivi majuzi, wamepokea barua kutoka kwa makao makuu ya wizara wakitaka Idara iteue wafanyikazi wawili wanaofanya kazi vizuri ili waende katika warsha itakayofanyika wakati wowote mwezi huo. Inafahamika kwamba baada ya warsha hii, wafanyikazi hao huenda wakapandishwa vyeo. Mkuu wa Idara anaagiza Kamau atekeleze matakwa ya barua hiyo.

Mutito Goigoi ambaye ni afisa katika Idara hiyo ni rafiki wa Kamau tangu utotoni. Maafisa kadhaa katika idara hii wamelalamika kuhusu tabia ya Mutito na pia kuhusu utendakazi wake. Mara nyingi Mutito hufika kazini akiwa amechelewa na pia huwa hachani nywele wala kunyoa ndevu zake. Nguo zake huwa zimejikunja kwa sababu hazipigwi pasi, ofisi yake huwa ndiyo chafu kwa zote katika idara yao, ikiwa na faili nzee ambazo zimetupwa ovyo ovyo kwa sakafu. Mutito akipewa kazi, hapeleki au haifanyi kwa wakati unaofaa. Hutumia asubuhi yote kusoma magazeti na kujaza fumbo la maneno katika jedwali mraba. Yeye ni mfidhuli na hana heshima kwa wananchi na pia wafanyakazi wenzake. Anaporudisha kazi aliyopewa, huwa ina makosa mengi. Mara nyingi, hubidi wafanyikazi wenzake katika Idara kurudia kazi yake. Mkuu wa Idara amemwonya Mutito mara kadhaa lakini hajabadilika.

Tangu aajiriwe, Mutito amebaki kuwa katika kiwango kile kile cha kazi na hamna dalili kwamba atapandishwa cheo hivi karibuni. Mutito anaenda kumuona Kamau kisha anamsihi amteue ili aweze kuhudhuria warsha hii kwa sababu huenda ikawa njia pekee inayoweza kutumiwa ili apandishwe cheo. Kamau anakubali kumsaidia mradi tu, Mutito amnunulie vinywaji kadhaa na nyama choma katika baa ya mtaa mwishoni mwa juma. Mutito anakubali. Kamau anaidhinisha Mutito ahudhurie warsha, anawaacha wafanyakazi wazuri wanaostahili kuhudhuria warsha hii. Mwishoni mwa juma, Mutito anatimiza ahadi yake kwa kumnunulia Kamau vinywaji kadhaa na nyama choma katika baa ya ‘Tukimbie Shida’.

Tangu wagundue kuwa Mutito ndiye aliyepewa nafasi ya kuhudhuria warsha, wafanyakazi wenzake wamekuwa na mwelekeo hasi kwa Idara na hawatii bidii katika kazi zao. Kwa sasa utendakazi wao katika Idara umedidimia.

Maswali:

1. ***Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?***

Aina kadhaa za uhalifu wa kifisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kamau alitaka Mutito amnunulie vinywaji na nyama choma ili amteue kama mojawapo wa wale watakaohudhuria warsha. Vinywaji hivi na nyama choma ni hongo. Mutito alimnunulia Kamau vinywaji na nyama choma ili amteue kuhudhuria warsha.

Kamau alitenda uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti. Kwa hivyo, ataweza kupatikana na hatia zifuatazo:

- Kuitisha hongo
- Kupokea hongo

Pia, Mutito amefanya kosa la hongo inayowahusisha maajenti kwa hivyo anapatikana na hatia ya kutoa hongo.

b) Kumdanganya mwajiri - kifungu cha 41 cha cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kamau anatenda uhalifu wa kudanganya mwajiri. Alifaa kupendekeza wafanyakazi wawili wenye ustadi teletele kuhudhuria warsha. Badala yake, aliteua mfanyakazi mzembe. Inawezekana kuwa Mutito hatatumia stadi atakazopata katika warsha kunufaisha Idara. Zaidi ya hayo, afisa wanaofanya kazi na Mutito wamevunjika moyo kwa sababu ya kitendo alichokifanya Kamau. Kitendo hiki kimesababisha utendakazi wa wenzake katika idara kudidimia.

c) Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kamau alitumia mamlaka yake vibaya wakati anapopendekeza Mutito ahudhurie warsha. Uteuzi wake haukujikita katika ustadi au ueledi. Kwa hivyo, alitumia mamlaka yake vibaya wakati alipompatia Mutito ambaye tabia yake ni mbaya nafasi ya kuhudhuria warsha. Kamau alimpatia Mutito nafasi hii kwa sababu alimwahidi vinywaji kadhaa na nyama choma.

2. ***Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?***

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Utovu wa kitaaluma – kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma kinamhitaji mtumishi wa umma kufanya kazi yake kwa njia ambayo itafanya umma kumuamini. Mutito anavunja sheria hii wakati anapokosa kuzingatia kazi yake.

Mifano Mahsusi

Katika sheria hii mtumishi wa umma anatarajiwa kufanya mambo yafuatayo:

- Kuwatumikia wananchi na watumishi wa umma wenzake kwa njia inayoonyesha adabu na heshima - Mutito anavunja sheria hii wakati anapokosa adabu na heshima kwa watumishi wa umma wenzake na wananchi.
- Kuvalia vizuri na kuwa msafi - Mutito anavunja sheria hii. Hachani nywele wala kunyoa ndevu. Nguo zake, kila mara ziilikuwa zimejikunjakunja kwa sababu hakuwa akizipiga pasi. Zaidi ya hayo, ofisi yake ilikuwa chafu kati ya zote katika idara nzima. Vilevile, ofisi hiyo ilikuwa na faili ambazo zimetupwa tupwa kila mahali sakafuni.
- Kuzingatia masaa ya kazi - mara nyingi, Mutito alienda kazini akiwa amechelewa na alitumia muda mwingi wa asubuhi kusoma magazeti. Kwa hivyo, amepotoka kitaaluma.

b) Kujitajirisha kwa kutumia mbinu zisizofaa – kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kifungu cha 11 katika Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma kinaeleza kuwa mtumishi wa umma haruhusiwi kutumia mamlaka yake kujitarajirisha. Watumishi wa umma hawaruhusiwi kupokea ‘zawadi’ kutoka kwa wale wanaowahudumia. Kamau alipata zawadi kutoka kwa Mutito. Mutito anamnunulia vinywaji na nyama choma ili ateuliwe kuhudhuria warsha. Kwa hivyo, anatenda uhalifu wa kujitajirisha kwa njia isiyo halali.

c) Mapendeleo ya kindugu – Kifungu cha 17 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kifungu cha 17 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma kinataja kuwa mtumishi wa umma hafai kupendelea kindugu au kufanya mapendeleo yoyote. Kamau alionyesha mapendeleo wakati anapoteua Mutito kuhudhuria warsha kwa sababu amekuwa rafiki yake kwa muda mrefu. Kwa hivyo, anatenda uhalifu wa mapendeleo ya kindugu.

3. Je, ungelikuwa Kamau, ungelifanya nini?

4. Je, ungelikuwa afisa katika idara moja na Mutito na unajua kuhusu mapatano kati ya Mutito na Kamau, ungelichukua hatua gani?

MFANO I

Injinia Mkora ni Mhandisi Mkuu katika mojawapo wa wizara serikalini. Ana habari kuhusu mradi wa barabara uliopendekezwa kwa sababu anashiriki katika upangaji wa barabara hii. Anataka kupata pesa kwa kuuza habari zisizoruhusiwa kwa umma, kwa kuwa haruhusiwi kumiliki kampuni ya ujenzi huku akiwa ameajiriwa na serikali.

Injinia anatafuta usaidizi kutoka kwake **Katikati** na **Kontraka** ambao ni wamiliki wa ***Maporomoko Construction Company Limited*** ili wamsaidie. Kabla ya zabuni kutangazwa rasmi kwa umma, anamwambia Katikati kuwa ana habari zisizoruhusiwa kwa umma ambazo zitamsaidia kupata zabuni. Injinia anamwambia kuwa akimpa habari hizo, anahitaji 'zawadi' ya asilimia tatu (3 %) ya malipo ya zabuni hiyo.

Injinia anajigamba kuwa anajuana na wanaotoa zabuni na pia ni mwanakamati wa kamati itakayojadili kuhusu zabuni hiyo. Kwa hivyo, atafanya kila awezalo kuhakikisha kuwa kampuni ya kina Katikati inapata zabuni hiyo. Wanakubaliana kuhusu hayo yote. Kisha kampuni ya ***Maporomoko Construction*** inapewa zabuni hiyo kama walivyopanga.

Injinia anakula njama na maafisa wa wizara kuu ili ateuliwe kuwa Mhandisi Mkaazi ambaye atakuwa akifanya kazi kwa niaba ya Mhandisi Mkuu. Anataka apewe kazi hii akisingizia kuwa ana maarifa kuhusu mradi huu kwa vile alihusika katika kupangwa na kuendelezwa kwa mradi. **Injinia** anateuliwa kuwa Mhandisi Mkaazi na wanaelewana kabisa na Kontrakta kwa sababu ya mafikiano walionayo kuhusu mradi huu.

Kama njia ya kutoa shukrani kwa Injinia kwa usaidizi wake, Kontraka ananunulia Injinia shamba kama 'zawadi' na pia anamjengea nyumba kubwa yenye bei ghali. Kontraka pia ananunulia familia ya **Injinia** mbuzi na ng'ombe kadhaa. Wanyama hawa wanafugwa kwa shamba alilomnunulia. Shamba na nyumba zinaandikishwa kwa majina ya bibi wa Injinia ili watu wasigundue mpango wao.

Miezi kadhaa baada ya mradi huu kuanza, Kontraka anamwambia Injinia kwamba pesa ambazo zilikuwa zimetengewa mradi huu zimeisha. Kwa hivyo, anataka pesa iliyopangiwa zabuni iangaliwe upya kisha pesa hizo ziongezwe. Katika kandarasi hii, **Injinia** ana uwezo wa kuidhiinisha pesa iongezwe.

Kontrakta anamsihi atumie uwezo alio nao kuongeza shilingi 100,000,000/- kwa mradi huu. Kama njia ya kuonyesha shurani, Kontrakta anaahidi **Injinia** na familia yake likizo ambayo atagharamia kila kitu ili waweze kutalii sehemu mbalimbali duniani. Mbali na hayo, anawaahidi pia zawadi nyinginezo. Kisadfa, Injinia amekuwa akitafakari jinsi atakavyopata zawadi nzuri ya kumpa bibi yake ili wakumbuke kuoana kwao kwa miaka 20 iliopita. Anaamini kwamba safari hii ya kutalii

itatatua hangaiko lake. Kwa hivyo, anakubaliana na Kontrakta. Injinia anapendekeza kuwa asilimia kumi iongezwe kwa malipo ya Maporomoko. Haya yote anafanya ili kuonyesha Kontrakta kuwa anakubaliana naye.

Punde tu baada ya Injinia kuidhinisha mipango yao, maafikiano yao yanajulikana kisha Wizara ya Barabara na Ujenzi na Wizara ya Fedha zinasimamisha malipo yoyote kwa kampuni ya Maporomoko. Wizara hizi zinataka uchunguzi ufanywe. Maporomoko inaorodheshwa kama kampuni mbaya na kuitwa 'kampuni danganyifu'. Uchunguzi unaanzishwa ili kujua jinsi Injinia alivyohusika katika mpango huu.

Unapofikia mwisho wa mwaka, Injinia kama mtumishi yeyote wa umma anatangaza mali yake. Hata hivyo, hakutaja shamba, ng'ombe na mbuzi au zawadi yoyote aliyopata kutoka kwa Kontrakta. Anaamini kuwa hahitaji kutaja mali hii kwa orodha yake kwa sababu imesajiliwa kwa jina la bibi yake.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) Ulaghai katika uwaniaji wa zabuni - Kifungu cha 44 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Injinia aliwapatia Katikati na Kontrakta habari zisizoruhusiwa kutangazwa hadharani. Kampuni nyingine ambazo zilitaka zabuni hazikupata habari hizi. Kwa hivyo, Kontrakta aliweza kuomba zabuni huku akizingatia masharti muhimu yanayozingatiwa kisha akapewa zabuni. Injinia, Katikati na Kontrakta wanatenda kosa la kufanya ulaghai katika uwaniaji wa zabuni.

b) Matumizi mabaya ya mamlaka – Kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Injinia ana habari kuhusu masharti yanayozingatiwa ili kampuni ipate zabuni kwa sababu yeye ni mtumishi wa umma. Anatumia mamlaka yake vibaya wakati anapotangaza masharti haya kwa kampuni ya Maporomoko ili Katikati, Kontraka na yeye wafaidike.

Injinia kama Mhandisi Mkazi ana uwezo wa kuidhinisha pesa za zabuni ziongezwe. Anatumia mamlaka yake vibaya wakati anapoongeza gharama isiyo halali kwa bajeti ya mradi kwa shilingi 100,000,000/-

c) Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Serikali ilimpa Injinia majukumu fulani na kwa imani kuwa atafanya kazi hiyo kwa uaminifu na pia kwa kuonyesha uwajibikaji. Alivunja uaminifu huu wakati alipohusika katika udanganyifu ili kutoa zabuni, kutumia mamlaka vibaya na pia kutumia maarifa yake kujinufaisha bila kujali matakwa ya umma. Kanuni za Uaminifu zinasisitiza kuwa watumishi wa umma wana jukumu

la kuwa waaminifu kwa niaba ya Wakenya. Wanatarajiwa kufanya kazi bila kupendelea, kuwa waaminifu, kuzingatia haki na kutekeleza majukumu yao kwa imani ya hali ya juu.

d) Hongo/ Hongo inayowahusu maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Uhalifu kadha wa hongo umetendwa katika kisa hiki:

Injinia

Injinia alimuuliza Katikati na Kontrakta wampe hongo ya asilimia 3 kwa malipo watakayopata kutokana na kandarasi ya mradi wa barabara kisha naye awape habari ambazo haziruhusiwi kutangazwa hadharani kuhusu zabuni. Injinia anatenda uhalifu ufuatao:

- Kuomba hongo
- Kupokea hongo

Injinia pia anapokea hongo ya shamba, mbuzi na ng'ombe na pia likizo iliyogharamiwa ya kutalii ulimwengu miongoni mwa vitu vingine. Anatenda uhalifu wa kupokea hongo.

Hongo si lazima iwe pesa.

Katikati

Katikati alikuwa mhusika mpatanishi katika mpango huu. Alipanga njama na Injinia na Kontrakta ili watoe hongo na pia wawahusishe maajenti katika hongo. Wanatenda uhalifu ufuatao:

- Kukubali kuomba hongo (kwa niaba ya Injinia)
- Kuahidi kupeana hongo (kwa niaba ya Kontrakta)

Kontrakta

Kontrakta alikubali kutoa hongo na pia aliahidi hongo. Kwa hivyo anatenda uhalifu wa hongo na hongo inayowahusisha maajenti. Haijalishi kuwa kitendo hiki hakikutendeka au kama sababu ya kuomba au kutoa hongo haikutimizwa. Kontrakata alimpa Injinia hongo ya asilimia 3 (3%) ili ampe habari muhimu zitakazomsaidia kupata zabuni. Pia alimnunulia Injinia shamba, ng'ombe, mbuzi na akamjengea nyumba. Kontrakata pia aliahidi kugharamia likizo yake ya kutalii ulimwengu.

Hata ingawa wizara ya fedha ilisimamisha kulipwa kwa shilingi million 100,000,000/- zaidi, uhalifu tayari ulikwishatendeka.

e) Kumdanganya mwajiri – Kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Injinia alipokubali kuangalia upya kandarasi na kuongeza shilingi 100, 000,000/- kwa njia isiyo halali na isiyozingatia sheria, alivunja sheria ya kudanganya mwajiri, yaani Wizara ya Barabara na Ujenzi na kwa hivyo serikali kwa ujumla.

f) Kuwasilisha habari za uongo au za kupotosha katika taarifa ya mali- vifungu vya 29 na 32 vya Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mbali na makosa ya ufisadi chini cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi, Injinia alikosa kwa sababu hakutoa habari za kweli, sahihi na zilizokamilika kuhusu mali aliyonayo yote, mapato yake, madeni na pia mali ya bibi yake na watoto wake wanaomtegemea kama inavyotakikana kisheria. Alifanya hivi ili afiche mali aliyopata kwa njia ya ufisadi. Haya ni makosa chini ya kifungu cha 32 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

g) Uhalifu wa kiuchumi – kifungu cha 45 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Injinia alisaidia Kontrakta kulipwa shilingi 100,000,000/- kutoka kwa serikali, kwa mradi uliokuwa wa uwongo na huduma ambazo hazikutolewa.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Kujitajirisha kwa kutumia mbinu zisizofaa – kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Injinia anavunja Kanuni za Maadili mema kwa kupokea ‘zawadi’ zinazoathiri maamuzi na majukumu yake.

b) Utovu wa utaalamu – kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Injinia alitarajiwa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utaalamu ili wananchi waweze kumpa yeye na ofisi yake heshima. Badala yake, Injinia aliidhinisha nyongeza ya pesa zilizofaa kulipwa Maporomoko ili naye apate ‘zawadi.’

c) Mamlaka ya sheria – kifungu cha 10 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kulingana na Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma, Injinia anapaswa kuzingatia na kuheshimu mamlaka ya sheria anapofanya kazi yake. Lakini anakosa kufanya hivyo.

d) Kutoa habari za uongo na za kupotosha – kifungu cha 19 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kwa kutoa habari za uongo kwa serikali kuhusu gharama ya mradi, Injinia anaongeza gharama ya mradi kwa shilingi 100,000,000/-.

3. Je, ungelikuwa Injinia, ungelifanya nini?

4. Je, ungelikuwa Katikati, ungelifanya nini?

5. Kama ungekuwa Katibu wa Kudumu katika Wizara anamofanya kazi Injinia, kisha habari hizi ziripotiwe kwako, ungechukua hatua gani?

6.Kama ungekuwa mwananchi kisha ujue maafikiano kati ya Injinia na Katikati, ungechukua hatua gani?

MFANO J.

Evario Mapesa ni mwenyekiti wa mojawapo wa Idara katika chuo kikuu cha **Fanya Bidii** ambacho ni chuo kikuu cha umma nchini Kenya. Idara hii inahitaji Mhadhiri Msaidizi kufuatia kujiuzulu kwa mhadhiri mmoja. Akili Nyingi, Mhadhiri katika chuo hiki anaenda kumwona Mapesa akitaka amwajiri ndugu yake anayeitwa **Ondoa Maarifa**. **Ondoa Maarifa** alihitimu kutoka chuo kikuu miaka miwili iliyopita na tangu wakati huo amekuwa nyumbani bila kazi. Alipopata habari kuhusu nafasi hii, **Ondoa**, anamsihi ndugu yake Nyingi atumie njia yoyote ile, hata kama ni kutoa hongo, ili apate kazi hiyo. Akili Nyingi anamwahidi kuwa atafanya kila awezalo kwa ajili hiyo.

Nyingi anampatia **Mapesa** vyeti vya **Ondoa** ili aangalie kisha ampe nafasi hiyo. Mapesa anaposoma vyeti hivyo kwa makini anagundua kuwa bali na kuwa Ondoa alisomea kazi tofauti, hakupita mtihani vyema. Mapesa anamweleza Nyingi kuhusu haya na kumwambia kuwa hawezi kumsaidia ndugu yake. **Nyingi** anamsihi **Mapesa** mara kadhaa ampe **Ondoa** kazi hiyo bila kufanikiwa. Mwishowe, Mapesa anakubali kumsaidia Akili iwapo tu Akili naye atuatumia 'akili' yake.

Siku moja asubuhi, Nyingi anazua tena jambo hilo kisha anampa Mapesa shilingi 20,000/-. **Mapesa** anakubali pesa hizi lakini anataka Nyingi aongeze shilingi 10,000/- zaidi akilalamika kwamba shughuli hiyo ni ngumu.

Katika mkutano wa idara uliofuata, inakubalika kuwa notisi iwekwe kwenye ubao wa matangazo wa chuo kikuu, ikitangaza nafasi hii, ili watu watume barua za kuomba kazi. Vilevile wanakubaliana kwamba barua hizo zitapokelewa na Mapesa ambaye atateua jopo la watu watatu ambao watawahoji waombaji kazi walioorodheshwa. Mapesa anaweka tangazo hili kwenye ubao wa matangazo kisha anateua jopo kazi huku akiwa mmoja wao. Wale wengine ni **Akili Nyingi** na Mwaminifu, ambaye ni Mhadhiri katika idara ya Mapesa.

Watu wengi walio na sifa zinazostahili wanatuma barua za maombi. Hata hivyo, wengi wao hawakuwekwa katika orodha teule ili wampe Ondoa nafasi nzuri ya kuweza kuchaguliwa. Wakati wa mahojiano, ni wazi kuwa kati ya wale wote waliohojiwa **Ondoa** ndiye aliyekuwa wa mwisho. Kwa hivyo, hastahili kupewa kazi. Mwaminifu anashangaa kabisa, wakati Mapesa na Nyingi wanamteua Ondoa kupewa kazi hiyo. Punde si punde, Ondoa anajiunga na idara ya Mapesa kama Mhadhiri Msaidizi.

Maswali:

1. ***Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?***

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) **Hongo / Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Mapesa na Nyingi wanashiriki uhalifu wa hongo inayowahusisha maajenti. **Nyingi** alimpa **Mapesa** shilingi 30,000/- ili atumie uwezo wake kumpa ndugu yake kazi. Uhalifu wa **Nyingi** unahusu mambo mawili.

- Kuahidi hongo
- Kutoa hongo

Uhalifu wa Mapesa pia unahusu mambo mawili:

- Kupokea hongo
- Kuomba hongo. Mapesa aliomba hongo ya ziada. Papo hapo anapomwahidi kumletea shilingi 10,000/- za ziada, anakubaliana naye.

b) **Kumdanganya mwajiri – kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Chuo Kikuu cha Umma kilidanganyika kikamwajiri Mhadhiri Msaidizi ambaye hajahitimu vilivyo. **Mapesa** na **Nyingi** wamefanya kosa la kumdanganya mwajiri. Wanatarajiwa kuzingatia utaratibu uliowekwa wanapowaajiri wafanyakazi. Badala yake, wanatumia udanganyifu na kumpa kazi Ondoa ambaye ndiye aliyekuwa wa mwisho kustahimili miongoni mwa wagombezi wenziwe.

c) **Mgongano wa maslahi –kifungu cha 42 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Mapesa na **Nyingi** hawakufaa kushiriki katika jopo la mahojiano kwa sababu maslahi yao yaliegemea kupatia Ondoa kazi. Hawakufichua ukweli huu ndiposa wote wanahusishwa katika jopo la mahojiano. Kwa hivyo wanatenda uhalifu wa mgongano wa maslahi.

d) **Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Mapesa alitumia mamlaka yake vibaya, alipotumia njia ya udanganyifu kuhakikisha kuwa **Ondoa** amepata kazi katika idara yake. Nyingi pia alitumia mamlaka yake vibaya kama mshiriki jopo, anapotumia udanganyifu kuhakikisha kuwa nduguye ameajiriwa kazi.

e) **Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 katika Sheria ya Adhabu *(Penal Code)***

Mapesa ameajiriwa na chuo kikuu na anatarajiwa kuwa mwaminifu. Chuo kikuu kinatarajia afanye kazi kwa nia njema, yaani bila udanganyifu lakini hakufanya hivyo. Mapesa na Nyingi wanavunja imani kwa sababu wanatarajiwa kutekeleza wajibu wao kwa njia ya

kweli na iliyo bora. Badala yake, walishirikiana kuwaondoa waombaji kazi waliohitimu kisha wakamchagua mwenye hakustahili kuwa Mhadhiri Msaidizi. Kwa kufanya hivi, wanafanya kosa la kukiuka imani.

2. ***Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umetendeka? Ikiwa kunao, ni upi?***

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) **Utovu wa utaalamu-kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.**

Mtumishi wa umma anatarajiwa kutekeleza wajibu wake kwa njia ambayo itaibua imani ya wananchi kwake na afisi yake. **Mapesa na Nyingi** walishiriki uhalifu huu kwa namna walivyotekeleza shughuli ya kuajiri.

b) **Kujitajirisha kwa kutumia mbinu zisizofaa -kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.**

Mtumishi wa umma hafai kutumia mamlaka yake kujitajirisha au kutajirisha wengine. Mapesa alivunja sheria hii alipopokea shilingi 30,000/- kutoka kwa Nyingi ili ampe Ondoa kazi**.**

c) **Mgongano wa maslahi - kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.**

Mtumishi wa umma anafaa kuhakikisha kuwa shughuli zake za kibinafsi hazihitilafiani na kazi rasmi aliyoajiriwa kufanya. **Mapesa na Nyingi** wanatenda uhalifu huu wakati wanapomtaka Ondoa aajiriwe kazi. Wanatawaliwa na matakwa yao ya kibinafsi na hivyo kutozingatia utaratibu unaofaa kumwajiri mfanyakazi.

d) **Uteuzi wa watumishi wa umma - kifungu cha 22 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.**

Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma inaeleza kuwa mtumishi wa umma anatakiwa kuendeleza kanuni au maadili ya kumteua mtumishi wa umma kwa kuzingatia kigezo cha uaminifu na ufaafu. Walimchagua Ondoa aliyekuwa na sifa za kiwango cha chini akilinganishwa na wagombezi wengine kwa sababu alitoa hongo.

3. ***Je, ungelikuwa Mapesa, ungelifanya nini?***
4. ***Je, ungelikuwa Mwaminifu, ungelifanya nini?***
5. ***Ikiwa wewe, kama mwananchi ungejua kilichotendeka, ungechukua hatua gani?***

MFANO K

Joe Mpotevu, rafikiye **Peter,** ni Afisa anayehusika na ununuzi wa bidhaa katika mojawapo wa mashirika ya umma hapa nchini. Peter na Joe wamekuwa marafiki wa jadi tangu walipokuwa wakisoma shule ya msingi. Kwa hakika, Peter ndiye aliyekuwa msimamizi wa Joe katika harusi yake na tangu wakati huo wamekuwa marafiki kifamilia. Peter anajua kwamba Joe anapata mshahara mdogo na imebidi mara kadhaa kuchukua mkopo ili awalipie ndugu zake karo ya shule. Joe ndiye kifungua mimba katika familia ya watoto wanane. Joe amekuwa na shida nyingi na mara kwa mara imebidi Peter amsaidie kulipa madeni yake.

Miezi minane iliyopita, **Omari Mjanja**, mhasibu katika shirika la umma alienda kumuona Joe akiwa na mpango wenye lengo la kuwatajirisha. Omari na Joe wanasajilisha kampuni yao, ***Mlaji Supplies***, ili wawe wakifanya ulaghai kwa kujidai kuuza bidhaa kwa kampuni hiyo. Joe ndiye anayeidhinisha vibali vya ununuzi wa bidhaa na Omari ndiye anayeidhinisha malipo. Mpango huu unahusu Joe kujifanya kuwa ameagiza bidhaa kwa niaba ya Shirika la Umma. Ukweli ni kuwa bidhaa hizi haziagizwi wala kupokewa. Omari anaidhinisha malipo ya bidhaa hizo kisha anaghushi hesabu ya vitabu vya shirika la umma ili kuhakikisha kuwa mpango wao haujulikani. Wanagawana pesa wanazopata kutoka kwa shirika hili zinazohusu bidhaa ambazo hazimo.

Joe ameweza kupata pesa nyingi kwa sababu ya udanganyifu huu. Amelipa madeni yake yote na hivi majuzi alinunua gari jipya aina ya Mercedez Benz. Kwa wakati huu anajenga maghorofa katika mtaa wa Wenye Pesa jijini. Vilevile, anapanga kujenga makazi yake mara tu akimaliza kujenga maghorofa. Peter ameshangazwa sana jinsi Joe alivyopata mali nyingi katika muda wa miezi minane. Mara kadhaa Peter amemuuliza Joe mahali anapopata pesa. Joe hajawahi kumpa jibu la kuridhisha. Peter anashuku kwamba Joe anahusika katika vitendo vya ufisadi.

Jioni moja, Joe anamtembelea Peter huku akionekana mwenye wasiwasi. Anamuomba amwekee *Mercedez Benz* yake kwa wiki chache huku akitafuta mtu anayeweza kuinunua. Joe anasisitiza kuwa lazima auze gari hilo haraka iwezekanavyo. Anamwambia Peter kuwa atampatia asilimia fulani ya pesa ikiwa atamletea mtu atakayenunua gari hilo. Kwa sasa, anaweza kutumia gari hilo atakavyo. Ingawa Peter anashangazwa na mambo haya, anakubali kufanya kama Joe alivyomsihi. Wiki moja baadaye, Peter anamjuza Ken Tafuta kwake Joe kama mnunuzi wa gari lake la *Mercedez Benz.*

Maswali:

1. ***Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?***

   Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

   a) **Kuhujihusisha na mali inayotuhumiwa kupatikana kwa njia isiyo halali – kifungu cha 47 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

   Peter anatenda uhalifu wa kuhusika na mali inayotuhumiwa kupatikana kwa njia isiyo halali wakati anapokubali kumwekea Joe *Mercedez Benz* yake. Kisha anaitumia kwa shughuli zake mwenyewe na baadaye akamleta Ken kwake Joe kama mtu anayeweza kununua gari lake. Haya yote anafanya huku akishuku kuwa Joe alipata gari hilo kupitia njia ya ufisadi.

   b) **Wizi – Kifungu 275 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)***

   Joe na Omari kupitia njia ya udanganyifu wanatumia pesa za shirika la umma kwa manufaa yao wenyewe. Waliiba pesa za Shirika la Umma. Kitendo chao ni kosa la ufisadi kama inavyoelezwa katika Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi, 2003.

   c) **Matumizi mabaya ya mamlaka – Kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

   Omari na Joe wanatumia mamlaka yao vibaya. Walishiriki katika kuliibia shirika la umma mapato yake.

   d) **Kukiuka Uaminifu – Kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)***

   Joe na Omari wanatarajiwa kufanya kazi zao kwa uaminifu ili shirika lao liweze kufaidika. Badala yake wanatumia njia ya udanganyifu kuliibia shirika lao. Wanasajili kampuni ambayo wanaitumia kupata malipo kwa bidhaa ambazo hazipo. Kwa hivyo, wanakiuka uaminifu.

   e) **Uhalifu wa kiuchumi – Kifungu cha 45 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

   Joe na Omari wanapata malipo kutoka kwa shirika la umma kwa bidhaa ambazo hawana. Malipo wanayopata kutoka kwa shirika la umma kwa bidhaa ambazo hawana, wanagawana kati yao wawili. Kwa hivyo wanatekeleza uhalifu wa kiuchumi.

2. ***Kama Omari angekujia akiwa na mpango kama huu, ungefanya nini?***
3. ***Je, ungelikuwa Peter, ungelifanya nini?***
4. ***Kama wewe ungekuwa mfanyikazi mwenziwe Joe kisha ujue kuhusu mpango huu, ungechukua hatua gani?***

MFANO L

Alois ni Afisa Mkuu katika kitengo kimojawapo cha utekelezaji wa sheria. Anafanya kazi katika eneo la dhiki. Ameoa lakini familia yake inaishi mahali pengine. Binti mmoja kwa jina Jane ametumwa hivi karibuni kama afisa katika kituo hicho. Jane anaishi na ndugu yake Bob ambaye ana umri wa miaka 17.

Alois amekuwa akitaka sana kuwa rafiki wa karibu wa Jane. Amemwelezea kuwa kama afisa msimamizi wa stesheni hiyo, ataamua mambo mengi kumhusu moja wapo ikiwa ni kazi zipi atapewa. Vilevile, anamkumbusha kwamba si rahisi kupata cheo kingine au nafasi za kupata mafundisho zaidi siku hizi, isipokuwa tu kama unajuana na mtu fulani. Anamfahamisha Jane kuwa afisa chipukizi na mrembo kama yeye hastahili kufanya kazi kwa makini sana wala hafai kusubiri kwa muda mrefu kama wengineo kabla ya kupandishwa cheo au kupata nafasi za mafundisho zaidi iwapo atashirikiana naye. Anaweza kupanga Jane ahamishiwe hadi kituo au kitengo cha utekelezaji wa sheria akipendacho. Anaongezea kwamba amewasaidia maafisa wengi wa kike kwa njia hiyo.

Hivi majuzi, Alois alimwita Jane katika afisi yake ili kumweleza kazi aliyotaka afanye. Baada ya kumwelezea Jane, akamwambia kuwa anampenda sana na angependa kumsaidia. Hata alijaribu kumkumbatia lakini Jane akatoroka kutoka ofisini mwake. Tangu kitendo hicho, Jane hapendi kuwa karibu na Alois. Jambo hili limeanza kuathiri utendakazi wake.

Alois ameanza kumpa Jane kazi ngumu na inayohatarisha maisha yake, huku akitarajia kwamba Jane atakubali matakwa yake. Alois, akiwa amekerwa kwamba Jane amekataa mambo yake, anapanga kukamatwa kwa nduguye Jane wa miaka 17 na maafisa wa polisi. Kwa namna fulani wanampata akiwa na bangi. Kila mtu anajua kuwa nduguye Jane ni kijana anayetii sheria. Alois anataka nduguye Jane apelekwe mahakamani kama njia ya kumwadhibu Jane.

Alois anamwita Jane kwa ofisi yake kisha anamwambia kuwa kesi ya ndugu yake si kubwa. Pia anamwelezea Jane kuwa ana uwezo wa kusuluhisha tatizo hilo. Anamtuma Jane nje ya ofisi ili afikirie kuhusu hali ya ndugu yake na jinsi anavyoweza kumsaidia.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Alois anatumia mamlaka yake vibaya wakati anapotaka kulala na afisa wa kike ili ampandishe cheo, amwajiri au aweze kumhamisha. Polisi waliomkamata ndugu ya Jane pia wanatumia mamlaka yao vibaya wanapomkamata, kumsumbua na kumtisha ilhali hana kosa lolote. Wanafanya haya kwa maagizo ya Alois.

b) Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Hongo si lazima iwe pesa. Yaweza kuwa kitu chochote kisichokuwa pesa. Joe anaitisha hongo anapotaka kulala na afisa wa kike ili awaandikie mapendekezo mazuri. Ikiwa afisa yeyote yule wa kike atakubali kulala naye ili apate cheo au nafasi ya kwenda kujifunza hiyo itakuwa ni hongo inayowahusisha maajenti.

c) Kumdanganya mwajiri – kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Alois ana cheo cha mamlaka. Maafisa ambao anawasimamia wanamtegemea yeye kuwaandikia barua za mapendekezo ili wapandishwe vyeo au hata pendekezo kuhusu jambo lolote kazini. Wasimamizi wakuu pia wanamtegemea kwa sababu wanatarajia apendekeze mtu fulani aajiriwe au apandishwe cheo bila kupendelea. Kwa hivyo, Alois atakuwa amemdanganya mwajiri ikiwa atapendekeza afisa fulani apandishwe cheo kwa sababu amelala naye iwapo afisa huyo hakuhitimu.

d) Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Mwajiri wa Alois anatarajia kuwa atafanya kazi kwa njia ya kweli na inayoonyesha uwajibikaji. Anatarajia kuwa atapendekeza afisa kupandishwa cheo, kupata uhamisho au hata kuajiriwa kazi bila kupendelea na pia kwa njia iliyo wazi. Alois anavunja uaminifu wakati anapotaka afisa wa kike wa kiwango cha chini kazini kulala naye.

Maafisa wa polisi wanamtungia uongo nduguye Jane kuwa ana bangi, kisha wanamkamata na kumfungia ndani, hawakufanya kazi kwa weledi na kwa hivyo wanavunja uaminifu kwa sababu wanatarajiwa kufanya kazi kwa uaminifu na uwajibikaji.

2. ***Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?***
   Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:
   a) **Utovu wa utaalamu – kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**
      Watumishi wa umma wanatarajiwa kufanya kazi zao kwa njia inayoonyesha uawajibikaji na pia kwa njia ambayo wananchi watawaamini. Kwa hivyo, Alois anatarajiwa kuonyesha wenzake wanaofanya kazi naye na wananchi heshima bila kuzingatia maumbile, kiwango chao cha kazi, kabila, tabaka, jinsia, imani, dini, utamaduni, lugha, ulemavu, au mvuto wa kisiasa.

   b) **Mapendeleo – kifungu cha 17 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**
      Mtu anapaswa kuajiriwa kwa kuzingatia uaminifu, ustadi au uwezo wake na pia kuhitimu kwake kwa kazi fulani. Hapafai kuwa na mapendeleo. Ili serikali iaminike, utaratibu wa kuajiri, kupandisha cheo au kupatia afisa zawadi yafaa usiwe na mapendeleo ili wananchi waiamini serikali. Joe alivunja sheria hii wakati alipowaajiri maofisa kadha wa kike, kuwapandisha vyeo au kuwahamisha kwa sababu wamelala naye. Matendo kama haya yanafanya watumishi wengine wa umma na wananchi kukosa imani katika serikali na pia kutoheshimu utawala wa sheria.

   c) **Unyanyasaji wa kijinsia – kifungu cha 21 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**
      Alois anamnyanyasa Jane kijinsia. Watumishi wa umma wamekatazwa kuwanyanyasa kijinsia wananchi au watumishi wenzao. Unyanyasaji wa kijinsia unahusu mambo yafuatayo, hata ikiwa anayeyafanya anajua hatakiwi kufanya hivyo au la:
      - Kumsaidia au kumpa mtu huduma huku ukitarajia kuwa baada ya kumsaidia utafanya mapenzi naye.
      - Kumshika mtu sehemu za mwili kimakusudi au ovyo ovyo kwa njia yoyote inayoonyesha unataka kufanya mapenzi naye.
      - Kufanya ishara, kelele, mzaha au kutoa maoni, kuhusu jinsia ya mtu fulani.

3) ***Ungempa Jane mawaidha gani?***

MFANO M

Dkt. Jembe Maarufu ni Msimamizi wa Matibabu katika Hospitali ya Wilaya ambapo **Dawa Kali** ndiye anayesimamia kitengo cha madawa naye **Tabitha Mzungu** akiwa Matroni. Hospitali hii ya wilaya ina vitanda 250, kitengo cha kujifungulia kina mama, chumba cha upasuaji na chumba kinachohifadhi maiti 20.

Wote watatu: Dkt. Maarufu, Dawa na Tabitha wanaendesha duka la kuuza madawa mita mia mbili kutoka kwenye lango kuu la Hospitali ya Wilaya. Duka hili la madawa hupata madawa na vifaa kutoka hospitali hii ya wilaya.

Juma, ambaye ni ofisa wa ununuzi na uuzaji wa mali ya umma, ndiye anayehusika na ununuzi na ugavi wa dawa na vifaa vya hospitali kutoka Shirika la Kutoa Vifaa vya Matibabu la Kenya. Mbali na kazi yake hospitalini, Juma pia huweka rekodi za fedha za duka la kuuza dawa la kibinafsi huku akipokea asilimia kumi na tano ya faida kutoka kwa duka hili. Hulifuatilia kila mara kuhakikisha kuwa duka hili la dawa la kibinafsi linapata madawa ya kutosha kutoka famasia ya Hospitali ya Wilaya. Kutokana na haya, famasia ya Hospitali ya Wilaya hukosa dawa na vifaa muhimu vya kiafya mara kwa mara.

Dkt. Jembe Maarufu kila wakati huwaandikia wagonjwa maagizo ya dawa ambazo anajua vizuri kwamba hazipatikani katika famasia ya hospitali. Wagonjwa hivyo basi, wanalazimika kutafuta dawa hizi mahali pengine. Naye **Dawa na Tabitha** kila wakati huwa wako karibu ili kuwaelekeza wagonjwa kwenda kwenye duka hili la dawa la kibinafsi ili wanunue dawa hizo.

Maswali:

1. ***Kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?***

   Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

   a) **Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

      Dkt. Maarufu, Dawa Kali na Tabitha Mzungu wote wametenda uhalifu wa matumizi mabaya ya mamlaka.

      - **Dkt. Jembe Maarufu** ametumia vibaya mamlaka yake kwa kutumia hospitali kuliuzia bidhaa duka lake la kibinafsi la dawa. Amewaandikia wagonjwa dawa ambazo zinaweza kupatikana tu katika duka lake la kibinafsi la kuuza dawa. Pia amechangia katika kuzoroteka kwa famasia ya hospitali kwa kuhamishia duka lake vifaa vya matibabu na dawa kutoka kwa famasia ya hospitali.
      - **Dawa na Tabitha** wametumia vibaya mamlaka yao kwa kuwaelekeza wagonjwa kwa duka lao la kibinafsi la dawa badala ya kuwapa dawa kutoka kwa hospitali.

- Juma ametumia vibaya ofisi yake kwa kupeleka madawa kwa duka la kibinafsi la dawa ilhali dawa hizi zilinuiwa kutumika kwa umma.

b) Mgongano wa maslahi – kifungu cha 42 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Dkt. Maarufu, Dawa Kali, Tabitha Mzungu na Juma wamefanya makosa ya mgongano wa maslahi. Wote wanafanya kazi katika hospitali ya wilaya na bado wanajihusisha na biashara ambayo ina ushindani wa moja kwa moja na famasia ya hospitali hii. Hawajawafahamisha wakuu wa hospitali kuhusu jambo hili na bado wanaendelea kuwaelekeza wagonjwa kwa duka lao la dawa ambalo linahujumu hospitali.

c) Hongo / Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Ili kupata ushirikiano wa Juma katika mpango huu, **Dkt. Jembe Maarufu, Dawa Kali na Tabitha** wanampa **Juma** asilimia kumi na tano (15%) ya faida kutoka kwa duka hili la kibinafsi la kuuza dawa. Juma anawasaidia kutunza hesabu na kuhakikisha kwamba bidhaa za dawa zinahamishwa kutoka kwa hospitali hadi kwa duka hili la kibinafsi la kuuza dawa. **Dkt Maarufu, Dawa na Tabitha** wana hatia ya hongo na hongo inayowahusisha maajenti.

d) Kumdanganya mwajiri- kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Dkt Maarufu, Dawa Kali, Tabitha na Juma wamefanya kosa la kumdanganya muajiri. Wamefungua duka la kuuza dawa la kibinafsi bila kuwaarifu wasimamizi wa hospitali, pale ambapo wanawatuma wagonjwa kununua dawa. Isitoshe, wameizorotesha famasia ya hospitali kwa kuhamisha madawa yaliyonuiwa kutumiwa na umma kwa duka lao binafsi.

e) Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Dkt. Maarufu, Dawa, Tabitha na Juma wana hatia ya kuvunja uaminifu. Wanahitajika kutekeleza wajibu wao kwa uaminifu na kwa manufaa ya hospitali na wananchi ambao wanawahudumia. Badala yake, wao kwa makusudi, wanatumia mamlaka waliyopewa kwa maslahi yao binafsi. Pia wamevunja maadili na kanuni za taaluma zao.

f) Uhalifu wa kiuchumi – kifungu cha 45 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Dkt. Maarufu, Dawa Kali, Tabitha na Juma wote wamefanya uhalifu wa kiuchumi ambao ni:

- Kuharibu mali ya umma. Kimakusudi, wanaibia famasia ya hospitali ili kulifaidi kibiashara duka lao la kuuza dawa.

- Kutumia fedha za umma katika kulipia madawa ambayo yanaishia kupelekwa katika duka la madawa la kibinafsi.

2. ***Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?***

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) **Utovu wa utaalamu - kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.**

Watumishi wa umma wanapaswa kutekeleza wajibu wa kazi zao kwa kuzingatia maadili ya kitaaluma. Wanafaa kutekeleza kazi hizo kwa njia ambayo itahifadhi imani na heshima ya umma kwao na afisi zao. Watumishi wa umma ambao ni wanachama wa vyama vya kitaaluma, pia wanatakikana kuzingatia maadili na kanuni za taaluma zao. **Dkt. Jembe Maarufu, Dawa Kali, Tabitha na Juma** wote wamekiuka sheria hii kwa mienendo yao.

b) **Kujitajirisha kwa njia isiyo halali - kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.**

Afisa wa Ununuzi na Uuzaji wa mali ya Umma amevunja Kanuni za Maadili kwa kupokea asilimia kumi na tano (15%) ya faida kutoka kwa duka la kibinafsi la kuuza dawa kama malipo ya kuweka hesabu za pesa na kupeleka dawa kwa duka hili, dawa ambazo zinatoka kwenye famasia ya hospitali ya umma, kinyume cha sheria.

c) **Mgongano wa maslahi – kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.**

Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma inasema kwamba mtumishi wa umma anapaswa kuhakikisha kuwa maslahi yake ya kibinafsi hayakinzani na majukumu yake ya kikazi. **Dkt. Jembe Maarufu, Dawa Kali, Tabitha na Juma** wote walikiuka sheria hii.

MFANO N

Mary alijiunga na Mpango wa Uboreshaji wa Kitaifa ambalo ni shirika la kiserikali la usalama zaidi ya miaka ishirini na mitano iliyopita. Polepole, alipandishwa vyeo na kuwa ofisa wa cheo cha juu katika shirika hilo. Miaka michache iliyopita alivumbua wazo jipya kwa manufaa ya shirika. Biashara ya Kampuni moja ya mabasi ya sehemu hiyo iliendelea kudidimia. Hata ingawa haikuwa na ushindani wa usafiri barabarani kwa muda mrefu, matatu sasa zilikuwa zinailetea ushindani mkubwa. Hata hivyo, matatu hizi hazikuwa na mpango mzuri na hivyo basi kukatokea wadhibiti biashara ambao walikuwa wakizuia wawekezaji wapya kuingia katika biashara hii.

Baada ya muda, Mary akalihusisha shirika hilo katika biashara ya usafiri pasipo na idhini au ruhusa kutoka kwa Bodi. Biashara hii ingeleta mapato zaidi kwa shirika na hivyo basi kusaidia kwa kuongezea fedha ambazo shirika lenyewe lingepewa na serikali. Hata hivyo, kwa kuwa hili ni shirika la usalama na biashara ya usafiri sio kazi muhimu ya shirika hili, ilibidi ununuzi wa mabasi ufanywe kwa siri.

Mary ana dadake anayeishi Uholanzi. Aliamua kumuuliza dadake afanye mipango ya siri na kampuni ya kutengeneza mabasi ya Uholanzi kwa lengo la kuipa kandarasi ya kuleta mabasi. Mary aliweza kushawishi shirika likaipa kampuni hiyo ya Uholanzi kandarasi ya kuleta mabasi. Kulingana na kandarasi hiyo, shirika hili lilipaswa kulipia mabasi haya kwa muda wa miaka 20. Kwa kuwa Mary alisaidia kampuni hiyo ya Uholanzi kupata kandarasi, kampuni hiyo ilikubali kuongeza bei ya mabasi haya kwa asilimia ishirini na tano (25%) kisha kumpatia Mary pesa hizo za ziada kupitia kwa dadake. Matokeo yake ni kwamba Mary aliweza kujinufaisha kwa pato dogo.

Mary alikuwa na kaka zake watatu ambao hawakuwa wameajiriwa na walikuwa wamekaa nyumbani kwake kwa muda wa miaka mitatu tangu watoke shuleni. Aliona kuwa biashara ya mabasi ya shirika ingekuwa chanzo cha ajira kwa kaka zake. Punde tu mabasi haya yalipoanza kufanya kazi, Mary alihakikisha kwamba kaka zake wameajiriwa kama Makondakta. Hakufichua kwa Meneja wa Uajiri kwamba hao walikuwa kaka zake. Mary aliwashauri kaka zake kuongeza mapato yao kwa kuiba pesa kidogo kutoka kwa nauli walizokuwa wakikusanya kila siku.

Mabasi haya yalipoanza kunawiri kibiashara, Mary aliweza kuwashawishi wasimamizi wa shirika kujenga nyumba za wafanyakazi, baadhi yao wakiwa Makondakta na madereva wa mradi huu. Mary alidhamiria kuwapa makazi kaka zake pindi nyumba hizi zikikamilika kwa sababu walikuwa washaanza kuwa wasumbufu nyumbani mwake. Kuhakikisha kwamba mradi huu wa nyumba umefaulu, Mary alifanya mpango shirika likanunua shamba lililokuwa karibu kwa shilingi 3,000,000/-. Mwenye shamba hilo amekuwa rafiki wa Mary kwa muda mrefu na alikuwa na matatizo makubwa ya kuuza shamba hilo. Kutokana na haya, mwenye shamba alimpa Mary zawadi ya 'shukrani' ya shilingi 100,000/-. Mradi wa ujenzi wa nyumba hizi ukaanza lakini

haukukamilika kwa sababu uliishiwa na pesa. Shirika halikuwa limefanya mpango au bajeti nzuri ya mradi huu. Ili kukamilisha ujenzi wa nyumba hizo, shirika lilihitaji shilingi bilioni 1.7 zaidi. Miaka michache baadaye, kampuni ya mabasi ikaporomoka. Sasa mabasi haya yameegeshwa katika uwanja wa shirika, mengi yao yakiwa yameharibika mno kwa sababu ya kuendeshwa vibaya.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

a) Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

- Mary alikuwa na upendeleo wa kindugu. Alitumia mamlaka yake kuwaajiri kaka zake kama manamba. Pia aliwapa ndugu zake ushauri wa kuiba kutoka kwa nauli walizokuwa wakikusanya.

- Mary pia alifanya mpango shirika likanunua shamba kwa njia isiyofuata kanuni. Alishawishi shirika kuanzisha mradi wa nyumba kwa minajili ya kuwapa malazi ndugu zake wasumbufu.

- Alitumia vibaya cheo chake kupata hongo kutoka kwa kampuni iliyoko Uholanzi.

b) Kumdanganya mwajiri – kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Mary alilipotosha shirika kuhusu gharama ya mabasi, gharama hii ilikuwa ni pamoja na hongo ya asilimia 25 aliyoipokea. Aliweka kifungu chenye kasoro kwenye kandarasi, kifungu ambacho kililifunga shirika kulipia mabasi kwa muda wa miaka ishirini. Hakulifichulia shirika kwamba baadhi ya malengo ya mradi wa mabasi na nyumba ulikuwa ni kuwatafutia kaka zake kazi na malazi.

c) Kukiuka uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Mary alitarajiwa kutekeleza wajibu kwa uaminifu, uwajibikaji na kwa manufaa ya shirika na umma kwa jumla. Kinyume na haya, alitumia cheo chake kujipendelea na kujinufaisha bila kuzingatia kanuni.

d) Mgongano wa maslahi – kifungu cha 42 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Mary alimtumia dadake aliye Uholanzi kupanga mambo ya ununuzi wa mabasi. Hata hivyo, hakufichua wajibu wa dadake katika kupanga shughuli hizi ambapo alijipatia hongo. Vilevile, aliwaajiri ndugu zake kama manamba bila kufichua uhusiano wake nao kwa meneja wa uajiri wa shirika.

e) Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Mary alitafuta na kupata hongo kutoka kwa kampuni ya mabasi ya Uholanzi. Haijalishi hata kama Mary aliipata kupitia kwa dadake. Mary na dadake pamoja na maofisa wa kampuni ya mabasi ya Uholanzi walijihusisha na kutoa hongo na kuwa maajenti wa ufisadi. Ni vyema kutambua kwamba hata kama dadake Mary anaishi nje ya Kenya, bado yuko chini ya Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi, na hivyo basi, anaweza kupelekwa mbele ya mahakama za Kenya kujibu mashitaka ya kupokea hongo. Mary pia alipokea hongo ya shilingi elfu mia moja kutoka kwa mwenye shamba ambalo liliuziwa shirika.

f) Uhalifu wa kiuchumi – kifungu cha 45 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

i) Kwa hiari, kutozingatia sheria au taratibu na miongozo inayofaa ambayo inahusika na ununuzi wa mali ya umma na usimamizi wa fedha – kifungu cha 45 (2) (b) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Mary alitenda uhalifu wa kiuchumi wa kukosa kwa hiari kuzingatia sheria na utaratibu unaofaa katika matumizi ya fedha za umma.

ii) Kujihusisha na miradi bila kuwepo kwa mpango wa awali - kifungu cha 45 (2) (c) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Mary alitumia pesa za umma kwa miradi ambayo haikuwa imepangiwa au kuwa na bajeti hapo awali. Hii ndiyo sababu kampuni ya mabasi ilisambaratika punde tu baada ya kuanzishwa kwa biashara hii. Mradi wa nyumba nao pia ulisimama.

iii) Kutozingatia taratibu za ununuzi wa mali ya umma na utoaji wa zabuni - kifungu cha 45 (2) (b) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

- Mary alifanya kampuni ya shirika kununua mabasi kwa siri bila kuwa na ushindani wa zabuni, hivyo basi kuzuia shirika kupata bei bora na thamani ya pesa.

- Pia alilifunga shirika na vilevile umma katika kulipa fedha kwa muda mrefu wa miaka ishirini bila idhini ya bunge kama inavyotakikana kisheria.

- Aligeuza fedha za shirika ili kulipia shamba lililokuwa karibu kwa kuwa alikuwa anamjua mwenye shamba hilo.

iv) Malipo ya kilaghai / yanayopita kiasi kutoka kwa fedha za umma – kifungu cha 45 (2) (a) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

- Mipango ya ununuzi wa mali ya umma ilifanyika kisiri na haikustahili kufanyika
- Bei iliongezewa kwa zaidi ya asilimia ishirini na tano ili kugharamia hongo ya Mary.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Utovu wa utaalamu –kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

Watumishi wa umma wanahitajika kutekeleza wajibu wao kwa weledi na kwa njia ambayo itavutia imani katika ofisi zao. Katika utendakazi wake, Mary alidhihirisha utovu wa utaalamu wa hali ya juu kabisa.

b) Kujitajarisha kwa njia isiyo halali –kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Watumishi wa umma wanakatazwa kutumia ofisi zao kujitajirisha. Mary alipanga, akatafuta na kupata hongo ya kiasi kikubwa cha pesa kutoka kwa kampuni ya Uholanzi. Pia alikubali zawadi ya 'shukrani' ya shilingi 100,000/- kufuatia ununuzi wa shamba lililokuwa karibu na shirika.

c) Mgongano wa maslahi -kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma inasema kwamba mtumishi wa umma atatumia juhudi zake zote kujizuia kuwa katika hali ambayo maslahi yake ya kibinafsi yatakinzana na majukumu yake rasmi. Mary alivunja sheria hii kwa kutumia dadake 'kupanga' biashara ya mabasi. Alivunja sheria hii pia wakati alipohakikisha kwamba kaka zake wameajiriwa kama manamba wa mabasi.

d) Kukosa kulinda mali ya umma iliyo chini yake - kifungu cha 15 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Watumishi wa umma wanahitajika kuhakikisha kwamba mali na ofisi za umma zinatumika kwa manufaa ya umma na sio kuendeleza manufaa yao binafsi au manufaa ya mtu mwingine. Rasilimali yote ya umma ni lazima itumike kisheria, kwa ufanisi, kwa njia inayofaa, kwa busara na kwa njia iliyokubaliwa. Watumishi wa umma wanawajibika kibinafsi kwa hasara yoyote au uharibifu wowote ambao utatokana na vitendo vyao kuhusiana na raslimali ya umma. Kutotunza na matumizi mabaya ya raslimali ya umma husababisha uharibifu na hasara. Mary hakulinda raslimali ya umma iliyokuwa chini ya mamlaka yake.

e) Mapendeleo ya kindugu - kifungu cha 17 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Uteuzi wote wa wafanyinyikazi unapaswa kufanyika kwa misingi ya uaminifu, uwezo na ufaafu. Ni lazima pasiwe na mapendeleo ya kindugu. Ili kudumisha uaminifu wa utumishi wa umma, taratibu za uteuzi, kupandishwa vyeo na kuwatuza wafanyikazi, lazima kuwe kwa misingi ya ustahili. Mary aliwaajiri ndugu zake huku akipuuza masharti haya.

MFANO O

Tume ya Uchaguzi nchini Kenya ilitangaza uchaguzi mdogo katika Wadi ya Usijali. **Jimmy Mlagai** ambaye ni mmojawapo wa wenyeji wa Wadi ya Usijali akaamua kugombea uchaguzi huu. Jimmy si maarufu katika wadi hii kwa sababu anatuhumiwa kuwa anahusika na visa vya uhalifu katika eneo hili. Kwa hivyo, sio rahisi kwake kuchaguliwa. Jimmy akiwa anajua haya, anaamua kuwahonga wapiga kura kwa unga wa mahindi, mafuta ya kupikia na leso ili aweze kushinda.

Andrew Mlegevu, ambaye ni binamu yake Jimmy anapata kazi kama Msimamizi wa Kituo cha Kupiga Kura katika uchaguzi huu. Jimmy anamwendea na kumwomba amsaidie kushinda. Anamwahidi Andrew zawadi nono kwa kazi hiyo. Andrew naye anakubali kumsaidia.

Wakati wa uchaguzi ambao ni kwa kura ya siri, Andrew anawachukua wazee na wale ambao hawajui kusoma na kuandika na kuhakikisha kwamba wanatia alama kwenye jina na ishara ya Jimmy, ambapo ni kinyume na mapenzi yao. Kufuatia haya, Jimmy anachaguliwa diwani wa Wadi ya Usijali. Wiki moja baadaye, Andrew anapokea shilingi elfu kumi kama zawadi ya 'shukrani' kutoka kwa Jimmy.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?

Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

Andrew amefanya makosa yanayohusiana na uchaguzi kinyume na kifungu cha 4 cha Sheria ya Makosa ya Uchaguzi.

a) Kuhonga maajenti – kifungu cha 10 cha Sheria ya Makosa ya Uchaguzi

Andrew na Jimmy wote wawili wamefanya makosa ya utoaji wa hongo kinyume na kifungu cha 10 cha Sheria ya Makosa yanayohusiana na Uchaguzi. Kosa hili pia ni ufisadi.

Andrew na Jimmy wote wawili, kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, waliwashawishi wapiga kura kupiga kura kwa njia fulani kupitia kwa:

- Kuwahonga wapiga kura kwa kuwapa unga wa mahindi, mafuta ya kupikia na leso;
- Kumwahidi Andrew hongo ili afanye hila katika uchaguzi;
- Kumpatia Andrew hongo ya shilingi 10,000/-

Andrew pia amefanya kosa linalohusiana na hongo. Katika kesi hii yake, kosa hilo lina mashtaka mawili:

- Kukubali kupokea hongo;
- Kupokea hongo ya shilingi 10,000/-

Wapiga kura wa Wadi ya Usajili ambao walipokea hongo ya unga wa mahindi, mafuta ya kupikia na leso kutoka kwa Jimmy, pia walifanya kosa linalohusiana na hongo. Wana hatia ya kupokea hongo.

b) Udanganyifu kuhusiana na uchaguzi wa watumishi wa umma - kifungu cha 4 cha Sheria ya Makosa ya Uchaguzi

Jimmy na Andrew walipanga njama ya kufanya udanganyifu katika uchaguzi huu kwa manufaa ya Jimmy. Andrew aliwapotosha wazee na wale ambao hawakujua kusoma na kuandika miongoni mwa wapiga kura kumpigia Jimmy kura. Wote wawili, Jimmy na Andrew wana hatia ya kutoaminika kuhusiana na uchaguzi wa watumishi wa umma.

c) Matumizi mabaya ya mamlaka - kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Andrew alitumia vibaya cheo chake kama Msimamizi wa Kituo cha Kupiga Kura kuhakikisha kwamba Jimmy amechaguliwa kuwa diwani.

d) Kukiuka Uaminifu– kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Kama Msimamizi wa Kituo cha Kupiga Kura, Andrew alitakikana kutekeleza majukumu yake kwa uaminifu na haki. Kwa kukosa kufanya hivyo, alikiuka imani.

2. Je, ni ukiukaji upi wa maadili ambao umefanywa?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Utovu wa utaalamu - kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Kama mtumishi wa umma, Andrew alitakikana kutekeleza kazi yake kwa njia ambayo inadumisha imani ya umma na uaminifu wa ofisi yake. Kwa kumsaidia Jimmy kuiba kura, basi alivunja sheria hii.

b) Mamlaka ya sheria - kifungu cha 10 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma anapaswa kufanya kazi yake kulingana na sheria. Andrew alivunja sheria alipomsaidia Jimmy kuiba kura.

c) Kujitajirisha kwa njia isiyo halali - kifungu cha 11 cha Sheria za Maadili ya Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma hapaswi kutumia ofisi yake vibaya kujitajirisha au kuwatajirisha wengine, na vile vile hapaswi kukubali zawadi isipokuwa tu iwe imekubaliwa kisheria. Andrew alivunja sheria hii alipokubali shilingi 10,000/- kutoka kwa Jimmy.

d) Mgongano wa maslahi - kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma atatia bidii kujizuia kuwa katika hali ambayo maslahi yake kibinafsi yanagongana na majukumu yake kirasmi. Andrew alivunja sheria hii wakati alipokubali kumwibia kura Jimmy binamuye.

e) **Kupotosha umma - kifungu cha 19 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**
Mtumishi wa umma, akiwa anajua, hapaswi kutoa habari za kupotosha kwa wananchi au kwa mtumishi mwingine wa umma. Kwa kuhakikisha kwamba wazee na wasiojua kusoma na kuandika wametia alama kwenye jina na ishara ya Jimmy wakati wa uchaguzi kinyume na matakwa yao, Jimmy na Andrew walivunja sheria hii.

f) **Uteuzi wa watumishi wa umma - kifungu cha 22 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**
Mtumishi wa umma anapaswa kutekeleza na kuendeleza kanuni mwafaka za uchaguzi na hasa kuhakikisha kuwa chaguzi zozote zimetekelezwa kwa haki. Kwa kumsaidia Jimmy kuiba kura, Andrew alivunja sheria hii.

3. ***Je, ungelikuwa Andrew, ungelifanya nini?***
4. ***Kama mpiga kura aliyeshuhudia kile Andrew alichokifanya katika kituo cha kupigia kura, ungechukua hatua gani?***

MFANO P

Ben Msimamizi ni Afisa Mkuu Mtendaji katika shirika la kiserikali nchini. Kama miezi miwili iliyopita, aliamua kujenga nyumba ya kifahari ya familia katika sehemu maarufu ya makazi jijini Nairobi. Aliposhindwa kugharamia mradi huu kwa pesa zake, Ben aliamua kuchukua kiasi fulani cha mapato ya shirika kugharamia mradi huu. Zaidi ya hayo, akaanza kuwa na safari nyingi za humu nchini na za nje ya nchi kwa kisingizio kwamba ni ziara za kikazi huku mara nyingi akichukua fedha nyingi za matumizi ili kutimiza nia hiyo. Hata hivyo ameshindwa kuelezea jinsi alivyotumia pesa hizo.

Ben pia ni mwanachama mwaminifu wa chama cha kisiasa cha **Tuendelee Mbele** Kenya. Ameshakuwa na nia ya kuendeleza azma yake ya kisiasa kwa kuwa mwenye kiti wa chama hiki. Ili kupata kuungwa mkono na wanachama, amebadilisha taratibu za kutoa zabuni ili kuhakikisha kwamba ni wanachama wenzake ambao wanapata zabuni kutoka kwa shirika. Kutokana na haya, wanaoliuzia shirika bidhaa wanahakikisha kwamba Ben anapokea asilimia fulani ya malipo wanayolipwa kama ishara ya 'shukrani.'

Ben angependelea kugombea kiti cha ubunge kwenye uchaguzi ujao. Kwa lengo hili, amewaajiri watu wengi kutoka kwa eneo bunge lake bila kufuata utaratibu uliowekwa. Anaamini kwamba hili litamfanya kuwa maarufu na litakuwa ni hakikisho la kupata kiti hiki cha ubunge katika uchaguzi mkuu.

Maswali:

1. ***Kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?***

   Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

   a) **Hongo / Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

      Kama malipo ya kukiuka taratibu za ununuzi wa mali ya umma na kuwazabuni wanachama wenziye katika chama chake cha kisiasa, Ben alipokea asilimia fulani ya fedha zote zilizolipwa wenye zabuni hawa. Ben na wauzaji bidhaa hawa wamefanya kosa linalohusiana na hongo.

   b) **Kudanganya mwajiri – kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

      Ben anatenda kosa la kumdanganya mwajiri kwa njia zifuatazo:

      - Kutumia mapato ya shirika kujenga nyumba yake badala ya kuyatumia mapato hayo inavyotakikana kisheria.
      - Kupokea kiasi kikubwa cha pesa kwa matumizi katika safari zake za humu nchini na za nchi za nje kwa kisingizio kuwa ni safari za kikazi, ilhali nia hasa ikiwa ni kujinufaisha kifedha.

- Kutumia ulaghai katika utaratibu wa ununuzi wa mali ya umma ili kuwapokeza wafanyibiashara walio wanachama wa chama chake cha kisiasa.
- Kuajiri watu kutoka kwenye eneo bunge lake bila kuzingatia ustahili au taratibu za uajiri zilizowekwa.

c) Mgongano wa maslahi – kifungu cha 42 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Ben ni mwanaharakati wa chama cha kisiasa cha Tuendelee Mbele Kenya. Badala ya kutangaza haya na kughairi kushiriki katika utoaji wa tenda pale ambapo wanachama wa chama hiki wanatuma maombi ya kupewa zabuni, Ben anakiuka utaratibu wa kutoa zabuni kwa kuwatunukia wanachama wenzake. Kwa hivyo anafanya makosa ya mgongano wa maslahi.

d) Hila katika utoaji wa zabuni – kifungu cha 44 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kwa kulaghai utaratibu wa kutoa zabuni katika shirika hili ili kuhakikisha kuwa ni wanachama wenzake ambao wanapata zabuni, Ben anafanya makosa ya hila katika utoaji wa zabuni.

e) Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Ben anatumia vibaya mamlaka yake kama Afisa Mkuu Mtendaji wa shirika kwa:

- Kutumia pesa za shirika kwa mradi wa kibinafsi wa kujenga nyumba;
- Kuchukua kiasi kikubwa cha marupurupu ambacho anashindwa kuelezea vilivyo matumizi yake;
- Kutoa zabuni kwa wanachama wa chama chake cha kisiasa;
- Kuajiri watu wa kutoka katika eneo bunge lake bila kufuata taratibu za uajiri zilizowekwa.

f) Kukiuka Uaminifu – kifungu cha 127 cha Sheria ya Adhabu *(Penal Code)*

Ben ana hatia ya kuvunja imani. Alipaswa kutelekeza majukumu yake kwa uaminifu na kwa manufaa ya shirika. Alikosa kufanya hivyo.

g) Uhalifu wa kiuchumi – kifungu cha 45 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Ben alitekeleza uhalifu wa kiuchumi. Alitumia vibaya fedha za shirika kwa kuzielekeza kwenye mradi wake wa kujenga nyumba yake. Pia alijipatia kiasi kikubwa cha marupurupu kwa kisingizio kuwa anasafiri nchini na nje kwa shughuli za kikazi, huku akishindwa kuelezea vilivyo matumizi yake.

2. Je, ni ukiukaji upi wa kimaadili umefanywa?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Utovu wa utaalamu - kifungu cha 9 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma ni lazima atekeleze majukumu yake kwa njia ambayo inadumisha imani ya umma kwa ofisi yake. Vitendo vya Ben vilikuwa kinyume na sheria hii.

b) Mamlaka ya Sheria – kifungu cha 10 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma anahitajika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Ben hakuzingatia sheria inayohusu utoaji wa zabuni, kuajiriwa kwa wafanyakazi na matumizi ya fedha za shirika.

c) Kujitajirisha kwa njia isiyo halali – kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma hapaswi kutumia ofisi yake kujitajirisha au kutajirisha wengine kwa njia isiyofaa; na hafai kukubali zawadi isipokuwa iwe imekubalika kisheria au na kanuni za shirika. Ben alipokea pesa kutoka wauza bidhaa na kutumia ushawishi wake kuwanufaisha. Kwa hivyo alivunja sheria hii.

d) Mgongano wa maslahi - kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma atatia bidii kujizuia kuwa katika hali ambayo maslahi yake ya kibinafsi yatagongana na majukumu yake ya kikazi. Ben alivunja sheria hii kwa kutumia cheo chake kushawishi utoaji zabuni, na kuajiriwa kwa wafanyikazi ambako kulikuwa kwa manufaa ya chama chake na watu wa eneo Bunge lake, mtawalia.

e) Kutopendelea upande wowote wa kisiasa - kifungu cha 16 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma, akiteleza majukumu yake, hapaswi kuendeleza maslahi ya chama cha kisiasa. Kwa kushawishi utoaji wa zabuni kwa mapendeleo ya wanachama wenzake, Ben amevunja sheria hii.

f) Mapendeleo ya kindugu -kifungu cha 17 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma hapaswi kuwa na mapendeleo ya kindugu. Ben alivunja sheria hii alipotumia ulaghai katika taratibu za utoaji zabuni ili kuwapatia zabuni wanachama wa chama chake cha kisiasa. Pia alivunja sheria hii kwa kuwaajiri watu wengi kutoka eneo bunge lake bila kujali taratibu za uteuzi.

g) Uajiri wa watumishi wa umma - kifungu cha 22 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Mtumishi wa umma anahitajika kuzingatia kanuni kwamba, watumishi wa umma ni sharti waajiriwe kwa misingi ya uaminifu, uadilifu na ufaafu. Kwa kuwaajiri watu wengi kutoka eneo bunge lake bila kujali taratibu za uteuzi, Ben alivunja sheria hii.

3. ***Kama mfanyikazi wa shirika hili, umegundua yale mambo ambayo Ben alikuwa akitenda. Je, ungechukua hatua gani?***
4. ***Kama mwananchi, umegundua vitendo vya Ben. Utachukua hatua gani?***

MFANO Q

Kauli Mnenaji ni Mhubiri Mkuu wa kanisa la **Kanisa Mlimani**. Kanisa hili limeanzisha mradi wa kujenga kanisa la kisasa kwa ajili ya waumini wake wapatao 2,000. Inatarajiwa kwamba gharama ya kujenga kanisa hili itakuwa shilingi 6,000,000/-. Kiasi hiki cha pesa kimetengwa kwenye bajeti ya mwaka ya kanisa.

Katika mkutano wa mashemasi wa kanisa wa kujadili mradi huu, inaamuliwa kuwa ilani za kualika zabuni ziwekwe kwenye vibao vya ilani vya kanisa. Pia inaamriwa kuwa matangazo ya kualika zabuni yafanywe katika ibada zote tatu za kanisa za Jumapili itakayofuata. Barua zote za maombi ya zabuni zapaswa kupelekewa Mhubiri Mkuu. Baadaye, Kauli angeitisha mkutano wa mashemasi kujadili zabuni hizi.

Binamuye **Kauli Mnenaji** anayeitwa **Biashara** ni kontrakta. Ana hamu ya kushinda zabuni hii na kwa hivyo anamwendea Kauli ili apate usaidizi. Kauli anakubali kumsaidia lakini kwa masharti ya kumkamilishia nyumba yake aliyokuwa akijenga huko mashambani. Ujenzi wa nyumba yake kauli umekwama kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Anahitaji shilingi milioni 3 kuikamilisha nyumba. Biashara anakubali kukamilisha nyumba hii kwa kutumia kiasi fulani cha pesa zilizotengewa ujenzi wa kanisa jipya.

Kufuatia ilani ya maombi ya zabuni, wajenzi wengi wametuma maombi yao ya zabuni ya kujenga kanisa. Kila anapopata zabuni hizi, Kauli anampatia binamuye **Biashara** habari muhimu kuhusu gharama na mahitaji mengine yaliyopokelewa kutoka kwa wajenzi pinzani. Kwa kutumia habari hizi, Biashara kila mara anabadilisha na kuboresha maombi yake ya zabuni. Biashara anapowasilisha maombi yake, yeye na Kauli wanaamini maombi yake ya zabuni yatafanikiwa.

Katika mkutano wa mashemasi unaongozwa na **Kauli**, maombi ya zabuni ya Biashara yanakubaliwa kwa kauli moja na anapewa kandarasi ya kujenga kanisa. Kauli anachangia katika mazungumzo ya mkutano huo lakini hasemi bayana kuwa **Biashara** ni binamuye.

Biashara anafika mahali pa kufanyia kazi na kuanza kazi mara moja. Ujenzi huu unapaswa kuchukua muda wa mwaka mmoja na inakisiwa kwamba, ibada za Krismasi za mwaka huo zingefanyiwa kwenye kanisa jipya. Hata hivyo, kufikia Oktoba, inadhihirika wazi kwamba **Biashara** hataikamilisha kazi hii katika muda uliowekwa.

Mnamo Novemba, **Kauli** anaitisha mkutano wa mashemasi kuwafahamisha kwamba **Biashara** ameishiwa kifedha na kwa hivyo hataweza kukamilisha ujenzi huu kwa muda uliokubaliwa. Anapendekeza kwao kufanyika kwa mchango wa harambee ili kutafuta shilingi 3,000,000/- za kuukamilisha mradi huu. Hata hivyo hafichui kwa mashemasi kwamba pesa nyingi zilizotengewa

mradi huu zilitumika kukamilishi ujenzi wa nyumba yake. Tayari Kauli amehamisha umiliki wa nyumba hiyo kwa mkewe baada ya makubaliano. Mashemasi wanaamua kwamba suala hili lijadiliwe na waumini wote katika mkutano maalum. Katika mkutano maalum waumini wanaonyesha kutoridhika kwao na mpango wa harambee na kukubaliana kwamba kazi ya kontrakta huyu ichunguzwe na kontrakta mwingine huru. Alfayo Meneja anateuliwa kutekeleza jukumu hilo.

Baada ya shughuli ya ukaguzi, Alfayo anagundua kuwa Biashara alitumia vifaa duni katika ujenzi huu bali na utendakazi wake kuwa mbaya. Maoni yake ni kwamba, ujenzi huu ungegharimu kiasi kidogo cha pesa kuliko 6,000,000/- ambazo Biashara alikuwa akiitisha.

Kwa kuwa Alfayo amegundua haya, Kauli na Biashara wanamwendea na kumwahidi shilingi 100,000 ili aandike ripoti inayowafaa. Pia wanamuuliza Alfayo aidhinishe kwamba shilingi 3,000,000/- zaidi zilihitajika kukamilisha ujenzi huu. Alfayo anakubali kufanya hivyo lakini kwa masharti kwamba aongezewe shillingi 150,000/- juu ya shilingi 100,000/- alizokuwa amepewa. Baada ya **Kauli** na **Biashara** kukubali masharti hayo, **Alfayo** anatoa ripoti inayopongeza kazi iliyokuwa ikiendelea na kushauri kwamba, 3,000,000/- zichangishwe kuukamilisha mradi huu. Ripoti inawasilishwa kwa waumini na matokeo yakawa kuwa mchango wa harambee ufanyike kutafuta shilingi 3,000,000/-. Kauli na Biashara wanampa Alfayo shilingi 150,000/- kama walivyokubaliana.

Maswali:

1. ***Kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?***

   Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

   a) **Hongo/ Hongo inayowahusisha maajenti – kifungu cha 39 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

      Kauli alitenda uhalifu wa kutoa hongo. Uhalifu katika mfano huu una mashtaka yafuatayo:

      - Kuomba kupewa hongo. Alimwuliza Biashara kumalizia mjengo wa nyumba yake ili naye amsaidie kupata zabuni.
      - Kupokea hongo. Biashara alikamilisha ujenzi uliokwama wa nyumba ya Kauli kama malipo ya kupewa zabuni kwa usaidizi wa Kauli.
      - Kukubali kutoa hongo. Kauli na Biashara walikubali kumpatia Alfayo hongo ya shilligi 100,000/-. Alfayo alipoitisha shilingi 150,000/- zaidi, walikubali kuzitoa.
      - Kutoa hongo. Kauli na Biashara walimpa Alfayo hongo ya shilingi 250,000/-.

      Biashara vilevile alitenda uhalifu unaohusiana na hongo. Katika kesi hii, uhalifu huu una mashtaka matatu:

      - Kukubali kutoa hongo. Biashara alikubali kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Kauli kwa malipo ya kusaidiwa kupata zabuni. Pia wakiwa na Kauli, walikubali kumpa Alfayo hongo ya shilingi 100,000/-.na Alfayo alipoitisha shillingi 150,000/- zaidi

kama hongo, alikubali.

- Kutoa hongo. Biashara alikamilisha ujenzi wa nyumba ya Kauli kwa malipo ya kusaidiwa kupata zabuni kutoka kwa Kauli.
- Kuahidi kutoa hongo. Alikubali kutoa hongo ya shilingi 250,000/- kwa Alfayo ili kushawishi Alfayo kuandika ripoti inayomfaa kwa waumini.

Alfayo alitenda uhalifu unaohusiana na hongo. Uhalifu huu una mashtaka matatu:

- Kukubali kupokea hongo. Wakati Biashara na Kauli walimwendea kwa pendekezo la kumpa hongo, alikubali kuipokea.
- Kupokea hongo. Alikubali hongo ya shiligni 250,000/- kutoka kwa Kauli na Biashara.
- Kuitisha hongo. Alidai aongezewe hongo ya shilingi 150,000/- zaidi ya ile alipokuwa anapewa na Kauli na Biashara.

b) Vishawishi vya kisiri kuhusu ushauri – kifungu cha 40 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kauli na Biashara kwa siri, walimhonga Alfayo ili atoe ushauri fulani kwa waumini ambao ungekuwa wenye manufaa kwao.

c) Kumdanganya mwajiri – kifungu cha 41 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kauli ametenda uhalifu wa kumdanganya mwajiri. Alipendekeza kanisa lifanye harambee ya kuchanga pesa za kukamilisha ujenzi wa kanisa jipya. Hata hivyo, alijua vyema kuwa pesa zilizotengewa ujenzi huu zilizidi kiasi kilichohitajika kukamilisha ujenzi, lakini zikatumika visivyo.

d) Mgongano wa maslahi – kifungu cha 42 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kauli alitenda uhalifu wa mgongano wa maslahi. Hakuwaambia mashemasi kuwa Biashara alikuwa binamu yake na akaendelea kushiriki katika majadiliano ya kutoa zabuni akijua kwamba anampendelea.

e) Ulaghai katika uwaniaji wa zabuni – kifungu cha 44 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Kauli na Biashara walitenda uhalifu wa hila za zabuni. Kauli alizifungua zabuni zilizokuwa zimewasilishwa na wauza bidhaa. Alimpa Biashara habari hizi. Kutokana na hayo, Biashara aliweza kuboresha maombi yake ya zabuni na mwishowe akashinda zabuni hii.

f) **Matumizi mabaya ya mamlaka – kifungu cha 46 cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Kauli alitumia mamlaka yake kujipatia faida kinyume cha sheria. Alimfanya Biashara kukamilisha ujenzi wa nyumba yake kwa pesa za kanisa ili naye Biashara anufaishwe katika ushindani zabuni. Kwa hivyo alitumia vibaya mamlaka yake.

2. Je, ungelikuwa Kauli kisha Biashara aje kwako akitaka msaada, ungelifanya nini?
3. Je, ungelikuwa Alfayo Meneja, ungelichukua hatua gani?
4. Kama ungelikuwa shemasi wa kanisa na ujue kilichokuwa kikiendelea, ungelifanya nini?
5. Ungelikuwa muumini na ukaja kujua yaliyotendeka, ungelifanya nini?

Katika kijitabu hiki cha kufundishia, mifano tuliyoisoma hadi sasa imetumika kuangazia makosa mengi ambayo ni ya ufisadi na hatia za kiuchumi chini ya Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi 2003 pamoja na Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

Kwa minajili ya kijitabu hiki, tutaangaziwa zaidi uhalifu wa kiuchumi na ukiukaji wa maadili katika mifano inayosalia.

MFANO R

Bw. Ogwanjo ni afisa wa cheo cha juu katika shirika moja la kiserikali mjini Nakuru. Mojawapo wa marupurupu yake kazini ni kupewa nyumba ya shirika yenye vyumba vitano vya malazi na yenye samani na vyombo vya matumizi. Hivi karibuni amekuwa mwandani wa Msajili wa Mashamba Wilayani anayeitwa Bw. Monke waliyefahamiana naye baada ya kuhudhuria mikutano, kongomano, na semina nyingi za kiidara.

Hivi karibuni, serikali imeamua kuuza nyumba zake ambazo hazikuwa na umuhimu mkubwa. Nyumba anayoishi Ogwanjo sio mojawapo wa zile zinazouzwa. Bw. Monke baada ya kupewa jukumu la kutafuta nyumba zitakazouzwa kisha kupeleka orodha hio kwa Kamishina wa Ardhi, ameorodhesha nyumba za Nakuru lakini hajapeleka orodha yake kwa Kamishina wa Ardhi. Bwana Ogwanjo anamwendea Bw. Monke kumwomba aiorodheshe nyumba aliyopewa na shirika katika orodha ya zile zinazouzwa. Bw. Monke anakubali kwa haraka huku akizingatia dhana kwamba huenda naye baadaye akahitaji usaidizi wake. Bwana Ogwanjo anatuma maombi ya kuidhinishwa ambayo yanakubaliwa na Monke na kutumwa Nairobi. Nyumba hii baadaye inauziwa Bwana Ogwanjo.

Bwana Ogwanjo anahitajika kulipa ushuru wa hati, ushuru wa ardhi, kodi ya ardhi na malipo ya kubadilishwa hati ya kumiliki shamba. Ukaguzi wa thamani ya nyumba ukiwa umefanywa na Mkaguzi wa Serikali, Bwana Ogwanjo anamwendea Bwana Monke ili ampe risiti ya bandia kwa Ushuru wa Hati wa shilingi 1,000,000/-, Ushuru wa Ardhi wa shilingi 50,000/-, na ya Kodi ya Ardhi ya shilingi 250/-. Kwa misingi ya risiti hizi bandia, mali hii inakabidhiwa Bwana Ogwanjo. Bwana Monke analipwa shilingi 100,000/- kwa usaidizi wake.

Maswali:

1. Kwa maoni yako, ni uhalifu upi wa kiuchumi ambao umetendwa?

Uhalifu kadhaa wa kiuchumi umetendwa. Huu ni pamoja na:

a) Kujipatia mali ya umma kinyume cha sheria – kifungu cha 45 (1) (a) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Nyumba hii haikuwa mojawapo wa zile zilizokuwa zimetengwa kuuzwa kwa kukosa umuhimu kwa shirika.

b) Kukosa kulipa ushuru – kifungu cha 45 (1) (d) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi.

Bwana Ogwanjo alishirikiana na Bwana Monke kupata risiti bandia za ushuru wa hati, ushuru wa ardhi, kodi ya ardhi na za malipo ya kukabidhiwa nyumba, hivyo basi kuinyima serikali mapato.

c) Kutozingatia sheria zinazofaa, kanuni na taratibu zinazohusu uuzaji wa mali ya umma – kifungu cha 45 (2) (b) Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

Bwana Ogwanjo na Bwana Monke walipanga njama ya kuiweka nyumba hiyo miongoni mwa zile ambazo hazikuwa na umuhimu mkubwa kwa shirika na ambazo zilikuwa zikiuzwa. Walifanya hivyo bila kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa.

2. Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) Mamlaka ya Sheria – kifungu cha 10 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Watumishi wote wa umma wanahitajika kufuata na kufanya kazi kulingana na sheria bila kujali vyeo na/au majukumu yao. Kwa kufanya nyumba iuzwe bila kufuata sheria na kanuni zinazofaa, Ogwanjo na Monke wamekiuka Mamlaka ya Sheria.

b) Kujitajirisha kwa njia isiyo halali – kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Ogwanjo amejitajirisha kwa njia isiyofaa kwa kutumia ofisi yake katika utumishi wa umma kupata mali na kwa hivyo amevunja Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

c) Mgongana wa maslahi – kifungu cha 12 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Ogwanjo amevunja kanuni zinazohusiana na mgongano wa maslahi kwa sababu alitumia ushawishi ili akabidhiwe nyumba.

d) Maadili ya kuendesha masuala ya kibinafsi – kifungu cha 20 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma

Ogwanjo na Monke wameshirikiana kumwezesha Ogwanjo aepuke kulipa ushuru na kodi zingine zinazofaa. Wote wamevunja Kanuni ya Maadili mema.

MFANO S

Tejpa ni mfanyi biashara mjini Thika. Anawaajiri wafanyakazi 1,000. Anapaswa kuwasilisha pesa wanazokatwa wafanyikazi kila mwezi za ***NHIF***, ***NSSF*** na ***PAYE***. Badala yake, amemwagiza **Mwangi,** ambaye ndiye **Afisa Ajira**, kuweka rekodi nyingine ya kuonyesha kwamba ana wafanyikazi ishirini (20) pekee. **Tejpa na Mwangi** wamekuwa wakiwasilisha pesa zinazokatwa kutoka kwa mishahara ya wafanyikazi ishirini pekee badala ya wafanyikazi elfu moja (1,000) ambao mishahara yao imekuwa ikikatwa kila mwezi.

Maswali:

Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote wa kiuchumi ambao umetendwa?

Ndio: Nao ni:

a) **Kukosa kulipa ushuru – kifungu cha 45 (1) (d) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Tejpa hajakuwa akiwasilisha pesa alizokuwa akiwakata wafanyikazi kwa Shirika la Kukusanya Ushuru nchini Kenya.

b) **Kukosa kulipa kodi – kifungu cha 45 (1) (d) Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

Kwa kukosa kuwasilisha malipo ya pesa zilizokatwa kutoka kwa mishahara ya wafanyikazi kwa Shirika la Malipo ya Uzeeni Kenya, Tejpa anatenda uhalifu wa kiuchumi.

Je, kuna ukiukaji wa maadili ambao umetendwa?

Tejpa na Mwangi sio watumishi wa umma kwani wanafanya kazi katika kampuni ya kibinafsi. Kwa hivyo, Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma haiwahusu moja kwa moja kwani inalenga kudumisha maadili miongoni mwa watumishi wa umma. Hata hivyo, wamekiuka maadili kutokana na vitendo vyao. Kuna haja ya kubuni na kutekeleza Kanuni za Maadili mema kwa mashirika ya kibinafsi na vyama vya kitaaluma.

MFANO T

Jilo ni Mtaalamu Mkuu wa Kompyuta anayesimamia mfumo wa orodha ya wapokea mshahara katika Baraza la Mji wa Mbula ambalo linawaajiri wafanyikazi 1,500. Kila mwaka wafanyakazi 10 hustaafu. Idara ya Huduma za Wafanyakazi humshauri Jilo kuondoa majina ya waliostaafu kutoka kwa orodha ya wapokea mshahara. Hata hivyo Jilo huondoa majina mawili tu na kubaki na yale mengine kila mwaka. Anahakikisha kwamba wale ambao majina yao yamebaki kwenye orodha, wanamwona kando ili awawezeshe kuendelea kupata mishahara yao. Wana mpango ambapo Jilo anapokea asilimia arobaini ya mshahara wa kila afisa ambaye amebaki kwenye orodha ya wapokea mshahara hata ingawa wamestaafu.

Kwa muda wa miaka kumi, vitabu vya mahesabu ya fedha vya Baraza la Mji wa Mbula havijakaguliwa. Hivi karibuni Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Fedha za Umma ameamrisha ukaguzi wa mahesabu ufanyiwe Baraza la Mji wa Mbula. Ukaguzi huu wa mahesabu umegundua makosa makubwa katika usimamizi wa fedha za baraza hili. Pia umeangazia hitilafu katika idadi ya wafanyikazi ambazo zilionyesha idadi kubwa ya wafanyikazi wamestaafu lakini wamebaki kwenye orodha ya wapokea mshahara.

Maswali:

1. ***Kwa maoni yako, kuna uhalifu wowote uliofanyika? Ikiwa upo, ni upi?***

   Aina kadhaa za uhalifu wa kiufisadi umetendwa. Aina hizi ni pamoja na:

   a) **Kujipatia fedha za umma kwa njia isiyo halali – kifungu cha 45 (1) (a) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

      Kwa kuchukua asilimia arobaini ya mshahara uliolipwa wale waliostaafu kinyume cha sheria na kwa njia ya ufisadi, Jilo pamoja na wafanyikazi ambao wamestaafu wamefanya kosa la kujipatia mali ya umma bila kufuata sheria.

   b) **Kukosa kuzingatia kwa hiari sheria, taratibu na kanuni zinazofaa – kifungu cha 45 (2) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

      Kwa kukosa kuondoa majina ya waliostaafu kutoka kwa orodha ya wapokea mishahara hata baada ya kuagizwa na idara ya kuajiri wafanyikazi kufanya hivyo, Jilo pia anafanya kosa la kukosa kwa hiari kuzingatia taratibu na kanuni kuhusu waliostaafu.

   c) **Kubadilisha kwa hila rekodi za kompyuta – kifungu cha 45 (1) (c) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi**

      Kinyume cha sheria, Jilo anaufanya mtambo wa kompyuta ufanye kazi kwa namna ambayo itapelekea shirika kupoteza mapato kwa kuendelea kuwepo kwa majina ya waliostaafu katika orodha ya wapokea mshahara.

2. ***Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?***

Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:

a) **Mamlaka ya Sheria – kifungu cha 10 cha cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**

Jilo amekiuka Mamlaka ya Sheria kwa kukosa kuzingatia taratibu zinazohusu usimamizi bora wa ustaafishaji katika Baraza.

b) **Kujitajirisha kwa njia isiyo halali – kifungu cha 11 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi kwa Umma**

Kwa kupokea asili mia fulani ya pesa ambazo zimelipwa kwa njia ya ufisadi kinyume cha sheria, Jilo amejitajirisha kwa njia isiyo halali na pia kuwatajirisha waliostaafu.

c) **Kutunza mali – kifungu cha 15 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma**

Jilo amekosa kutunza fedha za umma anazosimamia kwa kuendelea kutoa malipo kinyume cha sheria; kwa hivyo amevunja sheria hii. Atawajibika yeye binafsi kwa hasara iliyopatikana.

MFANO U

Bw. Kabu ni dereva katika Makao Makuu ya Wilaya ya Munyu ambapo anahusika na usafirishaji wa chakula cha msaada hadi kwenye sehemu zilizoathiriwa na njaa. Wakati wanapokuwa katika shughuli hizi za kupeleka misaada, wanalipwa marupurupu ambayo Bwana Kabu amekuwa akiyategemea mbali na mshahara wake. Kwa sababu ya kutoelewana na Afisa Mkuu wa Uchukuzi Bwana Asara, Bwana Kabu amesimamishwa kutoka kwa shughuli za kupeleka misaada na hivyo basi kupewa jukumu la kuwa mshika zamu usafiri nyakati za usiku, jukumu ambalo halipendi hata kidogo kwa sababu halina marupurupu.

Asubuhi moja anapotoka kazini anaingia kwenye ofisi ya Bwana Asara. Badala ya kurudisha ufunguo wa gari analoliendesha, anachukua funguo za magari yale mengine yaliyo kwenye maegesho na kuyafungua. Huku akiwa amejihami kwa pakiti mbili kubwa za chumvi, anamimina chumvi kwenye injini za magari haya na kwenda zake nyumbani huku akiwa ameridhishwa na kitendo chake cha kulipiza kisasi. Injini zote za magari haya matatu zinaharibika. Baada ya upelelezi, inagunduliwa kwamba Kabu ndiye alihusika na vitendo hivi.

Maswali:

1. ***Kwa maoni yako, ni uhalifu upi wa kiuchumi umetendwa?***

   Kuharibu mali ya umma – kifungu cha 41 (1) (c) cha Sheria dhidi ya Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi

   Kabu ametenda uhalifu wa kuharibu mali ya umma. Amesababisha uharibifu wa injini za magari matatu kwa kutumia chumvi na hivyo basi kuyafanya magari haya yasiweze kutumika.

2. ***Je, kuna ukiukaji wowote wa maadili ambao umefanywa? Ikiwa kunao, ni upi?***

   Ndio. **Ukiukaji wa maadili fulani umetendeka. Huu ni pamoja na:**

   Kutunza mali – kifungu cha 15 cha Sheria ya Maadili kwa Mtumishi wa Umma.

   Kwa kutumia chumvi kuharibu magari matatu, Bwana Kabu amekiuka kanuni ya maadili ya utendakazi kwa kutotunza mali ya umma. Atatakiwa kuwajibika kibinafsi kwa hasara iliyotokea.

ADHABU

Omuko ni mtumishi wa umma katika Wizara ya Ardhi. Kwamboka anamwendea Omuko kuomba msaada wa kupata shamba katika eneo zuri jijini. Omuko anakubali kufanya hivyo kwa maelewano kwamba Kwamboka atampatia shilingi 200,000/- kwa juhudi zake. Kwamboka anakubali naye Omuko anapanga kubadilisha umiliki wa shamba la umma na kulifanya la Kwamboka. Shamba hili liko katika eneo la Matajiri. Thamani ya shamba hili ni shillingi 2,000,000/- wakati lilipokuwa likibadilishwa umiliki.

Kwamboka anajenga jumba la kifahari katika shamba hili. Miezi mingi baadaye, serikali inatangaza

kwamba mijengo yote iliyoko kwenye sehemu zilizotengewa barabara itabomolewa ili kutoa nafasi ya ujenzi wa barabara za kando. Maofisa wa Wizara ya Barabara na Ujenzi wanamtembelea nyumbani Kwamboka na kutangaza kuwa jumba lake liko kwenye eneo lililotengewa barabara. Wanapendekeza kwamba jumba hilo lazima libomolewe. Kwa vile jumba hili limejengwa kwa vifaa vvenye nguvu, wizara inalazimika kukodisha buldoza ya kulibomoa. Kukodisha buldoza kunagharimu wizara hii shilingi 1,000,000/-. Omuko na Kwamboka baadaye wanakamatwa na kufikishwa mahakamani. Wanapatikana na makosa ya ufisadi na hatia za kiuchumi na hivyo basi kuhukumiwa kifungo cha miaka kumi gerezani pamoja na faini ya shilingi 1,000,000/- kila mmoja.

Tabia za Omuko na Kwamboka zilikuwa na faida na hasara zinazoweza kukadiriwa. Kwa hivyo, korti inaamua faini ya lazima ya kuongezewa itakayolipwa na Omuko na Kwamboka mtawalia. Faini ya lazima ni mara mbili ya kiasi cha faida iliyopatikana au hasara iliyotokea au mara mbili ya jumla ya kiasi cha faida au kiasi cha hasara ikiwa kitendo kilichopelekea kosa hilo kilileta faida na hasara.

Omuko alifaidika kutokana na hongo ya shillingi 200,000/- alizopokea. Kwamboka naye alifaidika kwa kupata shamba lenye thamani ya shillingi 2,000,000/- kinyume cha sheria ambayo ni hasara kwa serikali. Zaidi ya hayo, Wizara ya Barabara na Ujenzi ilipata hasara ya shilingi 100,000/- kwa vile ililazimika kukodisha buldoza, ambayo haingetokea kama Omuko na Kwamboka hawangevunja sheria. Jumla ya faida waliopata Omuko na Kwamboka ni shilingi 2,200,000/-. Jumla ya hasara iliyopata serikali ni shilingi 2,100,000/-. Kwa hivyo faini ya nyongeza ya lazima wanayotozwa Omuko na Kwamboka ni 2(2,000,000 + 200,000 + 2,100,000) = 8,600,000/- mtawalia.

Isitoshe, Kwamboka na Omuko wanawajibika kisheria kwa Wizara ya Ujenzi na Barabara kwa sababu ya hasara ambayo wizara ilipata ilipokodisha buldoza na kwa hivyo wanaweza kuulizwa kulipa kiasi cha shilingi 100,000/- pamoja na fidia.

Omuko akiwa mtumishi wa umma, pia yuko chini ya hatua za kinidhamu kutoka kwa usimamizi wake kwa sababu ya wajibu wake katika shughuli hii. Baada ya kushtakiwa kutokana na kosa hili, Omuko alisimamishwa kazi lakini alikuwa akipokea mshahara nusu huku matokeo ya kesi yakisubiriwa. Baada ya kuhukumiwa, aliendelea kusimamamishwa kazi lakini bila mshahara huku matokeo ya rufaa aliyokata yakisubiriwa. Alishindwa katika rufaa aliyokuwa amekata dhidi ya hukumu ya mahakama, na hivyo basi akafukuzwa kutoka kwa utumishi wa umma. Zaidi ya hayo, alikatazwa kuwa mtumishi wa umma kwa muda wa miaka kumi. Baadaye, Tume ya Kupambana na Ufisadi ya Kenya ilichapisha hukumu hii ya Omuko kukatazwa kuwa mtumishi wa umma kwa miaka kumi kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

TUME YA KUPAMBANA NA UFISADI YA KENYA
MAKAO MAKUU
Integrity Centre, Milimani / Valley Road Junction
S.L.P. 61130 - 00200, Nairobi
Simu: (020) 2717318, 310722, 2100312 / 3
Rununu: 0729 888881 / 2 / 3
Pepesi: (020) 2719757
Baruapepe: kacc@integrity.go.ke
Wavuti: www.kacc.go.ke

Kituo cha Kupokea Ripoti za Ufisadi
Simu za moja kwa moja: (020) 2717468, 0727 285663,
0733 520641
Pepesi ya moja kwa moja: (020) 2717473
Baruapepe: report@integrity.go.ke

AFISI YA TAWI LA MOMBASA
Apollo Court, Moi Avenue
S.L.P. 82351 - 80100, Mombasa
SIMU: (041) 2319081 / 2319082
Rununu: 0710 768 706
Pepesi: (041) 2319083
Baruapepe: kaccmsa@integrity.go.ke

AFISI YA TAWI LA KISUMU
3rd,Floor Jubilee Insurance House
Ang'awa / Oginga Odinga Street Junction
S.L.P. 438 - 40100, Kisumu
SIMU: (057) 2023111
Pepesi: (057) 2023555
Baruapepe: kaccksm@integrity.go.ke

www.kacc.go.ke

Chapisho hili katika lugha ya Kiingereza lilidhaminiwa na *Governance, Justice, Law and Order Sector Reform Programme (GJLOS)*
Wavuti: www.gjlos.go.ke

Chapisho hili katika lugha ya Kiswahili lilidhaminiwa na mpango wa *Kenya Institutional Support for Good Governance* wa *African Development Bank (ADB)*